# *KWA NINI?*

. . . muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu. Kila mmoja aliye na haja, na ijulikane kwa kumwinulia Mungu mkono wako. Shikilia haja yako moyoni mwako sasa, tunapoomba.

2 Mungu Mwenye Neema sana na Mtakatifu, tunakuja katika Uwepo Wako wa Kiungu sasa, kwa njia ya maombi, tukiomba kwanza kwamba utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe waliotukosea.

3 Basi kuna haja nyingi usiku wa leo, Baba. Unaiona mikono yao, na unajua shauku ya mioyo yao na kkilichoko humo ndani. Ningeomba pamoja, pamoja na mkono wangu ulioinuliwa, pia, kwamba Wewe ungetupa shauku ya moyo wetu, na hasa sana uponyaji wa miili yetu, na turudishiwe furaha ya wokovu wetu katika baraka nyingi sana za Mungu tunazotamani. Jalia ije juu yetu, Bwana.

4 Nasi tunaomba ya kwamba utawabariki wahudumu kila mahali, kote nchini na ulimwenguni kote. Kesho ikiwa ni sabato, na kutakuwako na makanisa na milango iliyofunguliwa, na watu wakija na kuondoka, na wahudumu wakihubiri na kuwaombea wagonjwa, Ee Mungu, tunaomba ya kwamba utamtia mafuta kila mmoja wa watumishi Wako kesho pamoja na jumbe kuu, na kusikia maombi yao kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Waokoe waliopotea, jitwalie Mwenyewe utukufu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

5 Mwaweza kuketi. Ni majaliwa makubwa sana kurudi maskanini, usiku wa leo, kuendelea kwenye usiku wa pili, ama, huu—huu, usiku wa tatu wa kukusanyika kwetu pamoja. Nasi tunasikitika kwamba hatuna nafasi ya kutosha ya kuketi kuwashughulikia hao watu wanaosimama kwa saa nyingi, tunajua viungo vyao vinauma. Lakini ninaomba kwa moyo wangu wote, kwamba Mungu wa Mbinguni atawapa thawabu kwa ajili yake katika ninii yenu . . . nanyi mnaosimama na kungojea jinsi mnavyongojea, huku wengi wenu mmeketi hapa wagonjwa na wahitaji.

6 Sasa, ndio kwanza nimwulize Billy Paul, mwanangu, na, kama Gene, ama yeyote wao, ama yeye mwenyewe aligawa kadi za maombi tena, naye akasema hawakuzigawa, kwa sababu tunatarajia, mara baada ya ibada usiku wa leo, ibada ya ubatizo. Chini kwenye orofa ya chini, naamini, ndipo kilipo kidimbwi.

7 Ninakumbuka wakati wa mwisho nilipokuwa hapa nao walikuwa na ibada ya ubatizo, ninaamini waliniingiza kisiri kwenye baadhi ya surupwenye za Ndugu Lyle. Yeye ni mrefu kidogo kuliko nilivyo mimi, kwa hiyo ilinibidi kuzikunja

miguuni, nao wakaniingiza kwenye kidimbwi hiki, kisha wakayatia maji moto sana, karibu yaniunguze. Lakini nilifanya kile nilichowazia kuwa ni sawa na kuwabatiza wote niliojua ningeweza kubatiza.

8 Sasa, kesho, ndiyo kwanza nisikie kutoka kwa Ndugu Moore ya kwamba ninapaswa kuzungumza baada ya shule ya Jumapili kesho asubuhi, mara baada ya ibada ya shule ya Jumapili.

9 Sasa, ninyi hapa mlio na makanisa mnayohudhuria, tusingependa mwikose ibada yenu wenyewe, ninyi simameni kwenye wajibu wenu. Sikuzote, wakati kanisa lenu lina ibada, mbona, nawe uko huku kwetu, mbona, ni jukumu lako kukaa kanisani mwako. Unaona? Na iwapo huna kanisa, na ungetaka kuja, mbona, tunathamini hilo.

10 Na basi wakati tunapowaombea wagonjwa, na kama una wapendwa, naamini, kama tu ungemwambia Mchungaji, "Itakuwa sawa kwangu kumpeleka Mama, Mwana, au mtu fulani huko kuombewa?" Nina hakika angesema, "Hilo ni sawa," unaona, kama unakuja kumleta mtu fulani aombewe.

11 Lakini laiti ungaliamini tu, mchungaji wenu ana mamlaka yale yale ya kuwaombea wagonjwa kama nilivyo nayo, mnaona, ama mtu mwingine yeyote. Haikubidi kwenda kwenye mkutano maalum upate kuponywa, hata si lazima uombewe, wewe mpokee tu, hilo tu ndilo linalohitajika.

12 Jana jioni Roho Mtakatifu alifanya jambo fulani maalum, hatukuwa na kadi zozote za maombi, kwa hiyo Yeye alipitia tu jengoni. Hilo si lilikuwa ni jambo la ajabu jinsi alivyofanya hilo?

13 Nanyi mnaona, uponyaji wa Kiungu haumo ndani ya mwanadamu, hata hivyo, mnaona, ni katika kazi iliyomalizika, imani yako katika kazi iliyomalizika. Basi karama ya uponyaji ni karama tu ya imani *kwa ajili ya* uponyaji. Mnaona? Sasa, karama ya uponyaji si lazima uwe, hata uwe ni mchungaji, inaweza kuwa m—mshiriki wa kawaida, walei wanaweza kuwa na kitu kile kile.

14 Mnaona, ninakumbuka wakati mmoja huko Meridian, Mississippi, naamini ndiko, nilikuwa nikifanya mkutano, na mvua ilikuwa inanyesha. Nilikuwa kule pamoja na mtu mmoja jina lake Brother, alikuwa mmoja wa wahudumu walioshirikiana, ama alikuwa ndiye aliyekuwa akiudhamini kupitia makanisa haya mengine, inaonekana kwangu kana kwamba jina lake lilikuwa ama Bigsbee, ama Busbee, ama kitu kama hicho, huko chini Mississippi. [Ndugu mmoja anasema, "Busbee."—Mh.] Busbee, labda huyo ndiye, mcheza kandanda, alikuwa, naam.

15 Na ilikuwa katika jumba la mikutano, ndipo ukaja ushuhuda ambao ulikuwa wa kustaajabisha, nao huo ushuhuda ulikuwa kwamba . . . Nilimtuma Billy aende kugawa kadi za maombi kusudi wasiufanye kama uwanja wa michezo, ni—ni kanisa. Ingawa ilikuwa ni ukumbi wa mikutano, lakini sisi, bado ni

kanisa mradi Kanisa linakutana pale. Kwamba popote pale ambapo . . . Watu ndio Kanisa, walioitwa watoke.

16 Ndipo ushuhuda ukaja baadaye, ya kwamba kulikuwa na maskini mama mmoja aliyeketi kwenye kiti cha mbele, maskini msichana wa kawaida tu wa kanisa, ambaye, maskini mama, na kulikuwako na mama mwingine akienda huku na huku akiwa na mtoto mchanga, naye huyo mtoto mchanga alikuwa amefunikwa blanketi, na mvua ilikuwa inanyesha. Maskini mama huyo hangeweza kupata mahali pa kuketi, ilikuwa tu imejaa na kusongamana hata mitaani, huku watu wamesimama na miavuli.

17 Na kwa hiyo, maskini mama huyu aliyeketi pale, Roho Mtakatifu akasema naye, mshiriki mdogo tu wa Mwili wa Kristo, naye akasema Roho Mtakatifu alimwambia, "Nenda, ukamwombee yule mtoto mchanga." Ndipo wakati mama huyo alipogeuka, alikuwa ameshika kadi ya maombi mkononi mwake.

18 "Lo," akasema, "Baba, si—siwezi kwenda kumwombea huyo mtoto, Ndugu Branham atamwombea huyo mtoto usiku wa leo," kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote nalo, bali akasema, "Ka—kamwe siwezi kumwombea huyo mtoto mchanga."

19 Basi wakati akitembea huku na huko, liliendelea tu kuingia moyoni mwake zaidi na zaidi, "Nenda ukamwombee huyo mtoto!"

20 Basi, hatimaye, akasema, "Pengine, labda, kuliondoa moyoni mwangu, ninaweza tu kumpa mama huyu kiti changu, kwa vyovyote vile, kwa sababu anaonekana kama amechoka."

21 Naye akasema ya kwamba alisema, "U hali gani, Dada?" Kasema, "U—unaonekana umechoka sana na huyo mtoto mchanga, na mi—mimi sijachoka, sina mtoto wangu mchanga, kwa hiyo waweza tu kuchukua kiti changu na kuketi hapa chini?"

Naye akasema, "Loo, asante, Dada, sitaki kuchukua kiti chako."

22 Akasema, "Naam, lazima ukichukue, kwa sababu na—naona kwamba umechoka na umedhoofika." Vema, akaketi chini. Akasema, "Kabla tu hujaketi," kasema, "naona ya kwamba una kadi ya maombi mkononi mwako."

Kasema, "Naam, huyo kijana alinipa hiyo dakika chache zilizopita, alipokuwa akitoka mlangoni."

Kisha kasema, "Vema, Ndugu Branham atamwombea mtoto wako mchanga, usiku wa leo."

Akasema, "Natumaini hivyo. Natumaini namba yangu itaitwa usiku wa leo."

23 Naye akasema, “Loo, ni—nitaomba ya kwamba Ndugu Branham ataiita namba yako, usiku wa leo.” Na kisha akasema, “Kama mimi, nikiwa Mkristo, siwezi kuliondoa moyoni mwangu kwa hiyo kama utaniwia radhi, ingekuwa, ingetuliza hisia zangu kama ungeniruhusu tu nimwombee dua ndogo mtoto wako mchanga.”

“Mbona,” akasema, “Hakika, kipenzi, endelea, mwombee mtoto.”

24 Ndipo akamshikilia naye maskini huyo mama akamwekea mikono huyo mtoto mchanga akilia, na kusema, “Bwana, na—na—nafanya jambo hili, kusudi niliondoe moyoni mwangu. Ninaomba ya kwamba utamponya huyu mtoto wakati mtumishi Wako, Ndugu Branham, atakapokuja na kumwombea, jalia aponywe.”

25 Ndipo akaketi chini, yule mama mwingine mwenye mtoto, naye mama huyu akaenda na kupanda juu kabisa kwenye roshani, ninaamini ilikuwa na roshani mbili, naye alikuwa kwenye roshani ya juu.

26 Kwamba yapata dakika tano baada ya hayo nikaingia, na baada ya kumaliza kuhubiri nikasema, “Nitaita kadi za maombi namba ishirini na tano hadi hamsini,” ama kitu kama hicho.

27 Mnajua jinsi ninavyofanya kwa kawaida, huanzia mahali fulani, ambapo kadi zimechanganywa na kuliita tu kundi moja kusudi watu wasisongamane, “Ninachukua namba moja,” ama, “namba mbili,” ama chochote kile.

28 Basi ilitokea kwamba mama huyu alikuwa karibu wa tatu au wa nne mstarini. Vema, maskini huyo mama huko juu jengoni, mwajua, huko juu, alikuwa na furaha sana, akasema, “Loo, asante, Bwana. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya maskini mama huyo, aliyekuwa moyoni mwangu *sana*, kwa ajili ya maskini mtoto huyo mchanga, mgonjwa.”

29 Wakati maskini huyo mtoto mchanga alipoingia kwenye mstari wa maombi, akaja karibu na mahali tulipokuwa tumesimama, mahali nilipokuwa nimesimama, nikamwangalia, sasa, tunalo kwenye kanda, mwajua, na kusema, hivyo ndivyo nilivyolishika, Naye akasema, “Dada,” kasema, “mtoto wako ana—anaugua,” ninasahau ilikuwa ni nini, namna fulani ya ugonjwa, ama shida. Kasema, “Unatoka mahali fulani, nawe ni *Fulani-wa-fulani*, Bibi *Jina fulani*,” na kusema, “lakini mtoto wako tayari ameponywa.” Kasema, “Kwa sababu Roho Mtakatifu alinena na maskini mama yule aliyesimama pale kwenye roshani, tayari ameomba maombi ya imani kwa ajili ya mtoto wako mchanga.” Mnaona?

30 Huruma ya mama huyo kwa huyo mtoto mchanga ingalikuwa kubwa sana kuliko ile ningalimwonea, mnaona. Kwa hiyo karama ya uponyaji, kama Mungu kamwe akinena na moyo wako uende ukamwombee mtu fulani, wewe fanya yale

Mungu anayokwambia ufanye, unaona. Unaona? Daima mfuate Roho Mtakatifu.

31 Jana usiku, tukizungumza. . . Tunaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Mnaamini hilo, sivyo? Kabla tu ya kuja kwa Bwana Yesu. Na halafu jinsi ambavyo Mungu hapo mwanzo, wakati Yesu alipokuja duniani, Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, bali nikizifanya kazi za Baba Yangu, basi ziaminini hizo kazi." Kama usingeweza kumwamini Yeye kama Mwanadamu, mbona, amini kazi zinazomfuata huyo Mtu.

32 Nasi tuliona tukizungumza jana usiku, ya kwamba Mungu kwanza alijifunua Mwenyewe katika Nguzo ya Moto, kisha akajifunua Mwenyewe katika Mwanawe, sasa anajifunua Mwenyewe katika Kanisa. Mnaona? Mungu yeye yule, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, unaona, ndani ya Kanisa. Vema. Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, ndivyo ilivyo.

33 Sasa, halafu tunaona ya kwamba Yesu alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli. Vema, alipokufa, akazikwa, akafufuka, na kupaa Juu, tunatambua ya kwamba Mungu, ya kwamba yule Logos, ama ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli nyikani, Huyo alikuwa ni Kristo, Huyo alikuwa ni ule Upako.

34 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Ninapenda Neno hilo, *MIMI NIKO*, nanyi je? Si, "Nilikuwa," au, "Nitakuwa." "MIMI NIKO." Kama ukisema siku za miujiza zimepita, unamfanya aseme, "Nilikuwa," bali Yeye hakusema hivyo. "MIMI NIKO. Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."

35 Sasa, tunaona basi ya kwamba wakati Yeye, baada ya kufufuka Kwake na kupaa, alirudi kwa Mungu ambaye Yeye alikuwa, ambaye aliwaongoza wana wa Israeli nyikani, Naye alikuwa ni Nguzo ya Moto tena.

36 Paulo, akienda zake Dameski, alibwagwa chini na Nuru, wala hakuna mmoja wa hao wengine aliyeiona Nuru hiyo, ila Paulo aliiona. Basi alipobwagwa chini, alisikia Sauti ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Naye akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Alitoka kwa Mungu, Naye akaenda kwa Mungu.

37 Tunaona ya kwamba katika siku hii ya mwisho Roho Mtakatifu amerudi katika huduma ya Kipentekoste, tuna picha Yake, Nguzo ile ile ya Moto. Sasa, Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwako wakati huo, ambayo ilidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, na, ikaonyesha ishara ya Masihi kwa watu. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi kama tulivyojifunza, ile ishara ya Masihi, Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii.

38 Huyo ndiye Israeli wote wa kweli wamlitazamia, alikuwa ni nabii, kwa sababu kwamba Mungu alikuwa amesema, "Akiwepo mtu miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana, nitajitambulisha Mwenyewe kwake, na yale asemayo yakitimia, msikieni, niko pamoja naye; yasipotimia, basi msimsikie."

39 Naye Musa akasema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi." Nasi tunaona ya kwamba wakati Yesu alipokuja, ya kwamba alifanya ishara ya nabii mbele ya mtu aliyeitwa, hebu tuseme Simoni Petro. Jina Lake lilikuwa Simoni wakati huo, Naye akasema, mara alipomwendea, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, utaitwa Petro; baba yako alikuwa ni Yona." Loo, huyo alikuwa ni yule Nabii kabisa!

40 Naye Nathanaeli akaona jambo hilo, na, ama, Filipo akaliona, akakimbia akamwambia Nathanaeli, "Njoo, umwone Yule tuliyemwona, ama, Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

Naye akasema, "Laweza jambo lolote jema kutoka. . .?"

Akasema, "Njoo, uone."

41 Hapana shaka alimsimulia hadithi ya jambo hilo alipokuwa akivuka. Basi Nathanaeli akiwa ni Mwebrania hodari na mwaminio, mara tu alipoingia kwenye mstari wa maombi, ama kusanyiko popote pale, vema, tunaona ya kwamba Yesu alisema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Akasema, "Rabi, ulinijua lini Wewe?"

Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Hilo lilitosha, akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli."

42 Sasa, kuna jamii tatu za watu duniani, kama unaamini Biblia, kuna jamii tatu tu, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Petro akiwa na zile funguo wakati wa Pentekoste aliwafungulia Wayahudi; Filipo alishuka akaenda kuhubiri na akawabatiza huko Samaria, lakini Petro akashuka, akawawekea mikono, wakampokea Roho Mtakatifu; na nyumba ya Kornelio, alikuwa na funguo zilizowafungulia hawa watu watatu.

43 Sasa, kulikuwako na jamii mbili za watu zikimtazamia Masihi kuja, Msamaria na Myahudi. Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Hiyo ni kweli? "Jua la haki," wale wanaomtazamia, "litazuka katika—katika wakati wa mwisho, uponyaji katika mbawa zake."

44 Sasa angalia, sasa, wakati alipojitambulisha kwa Wayahudi kwa ishara Yake ya Masihi. . .Hana budi kupitia Samaria, alikuwa na haja, ingawa alikuwa anaenda Yeriko. Ndipo huyo

mwanamke akatokea, tunajua hadithi hiyo, jinsi alivyowasiliana na roho yake kwanza, na akaanza kuzungumza naye, na kusema, “Nipe maji ninywe.”

Na mazungumzo, kulikuwa na ubaguzi, akasema, “Si kawaida.”

Na baada ya kitambo kidogo akapata shida yake ilikuwa ni nini, akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

45 Yeye . . . akasema, “Umesema vema,” Yeye alimwambia hivyo, “kwa kuwa umekuwa na waume watano, yule unayeishi naye sasa siye mume wako, kwa hiyo umefanya vema.”

Akasema, “Bwana . . . ”

46 Angalia tofauti kati yake na hao makuhani, marabi, wao walisema, “Yeye ni Beelzebuli,” wakati alipofanya hivyo. Nao wakasema . . .

Akasema, “Hilo halisameheki.” Kumwita Roho wa Mungu kitu kichafu, ni kukufuru. Mnaona?

47 Lakini mwanamke huyu alijua mengi zaidi kuhusu hiyo huduma kuliko wahubiri wengi wanavyojua siku hizi. Hiyo ni . . . Ingawa tunafikiri alikuwa ni kahaba, lakini alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe u Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye ataonyesha mambo haya.” Alikuwa amefunzwa, alijua alichokuwa akitazamia.

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

48 Juu ya hili akaacha mtungi wake wa maji na kukimbia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi? Si hivyo ndivyo Masihi anavyopaswa kufanya?”

49 “Naam.” Nao hao watu wakamwamini Yesu kwa sababu ya msemo wa yule mwanamke kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu Yeye alionyesha ishara ya Masihi.

50 Sasa, hakuna hata wakati mmoja katika Maandiko alipowahi kuwafanyia hilo Mataifa, la. Lakini Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa, na katika siku za Lutu.” Sasa, tulilichukua . . . Angalia, katika siku za Lutu kulikuwako na matabaka matatu ya watu. Sikuzote kuna matabaka matatu, kila kitu kiko katika utatu, na utatu kwa moja.

51 Angalieni, kulikuwako, katika siku za Lutu kulikuwako na asiyeamini, Wasodoma; kulikuwa na Lutu, lile kanisa vuguvugu, na familia yake; kulikuwa na Ibrahimu, aliyeitwa atoke, ameketi jangwani kwa hiari yake. Si kwa sababu ilimbidi kufanya hivyo, bali kwa hiari yake alishika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa.

52 Wakati wale Malaika waliposhuka na kunena naye, walikuwa . . . Ninaamini ilikuwa ni Theofania, kweli ninaamini, kwa sababu ilikuwa ni Mungu. Wawili wao, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika, walishuka wakaingia Sodoma, na kuwahubiria Wasodoma na kanisa vuguvugu. Wala hawakufanya miujiza yoyote, ila tu waliwapofusha. Na kuhubiri Injili humpofusha asiyeamini, tunajua hilo. Kuhubiriwa kwa Neno humpofusha yeye asiyeamini.

53 Lakini angalieni ishara ambayo Malaika huyu alifanya huko nje kwa Kanisa teule, alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, naye alikuwa ni Mgeni, ndipo akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Hiyo ni kweli? Akamwambia alikuwa ameoa, na jina la mke wake lilikuwa Sara, Mgeni.

54 Basi angalieni, Biblia inasema hasa, "Yuko hemani nyuma Yako," nyuma ya huyo Mtu. Mungu akidhihirishwa katika mwili, Mtu huyu alidhihirishwa. Ibrahimu alimwita Elohimu, Mwenyezi. Mnaona yale atakayofanya katika siku za mwisho? "Hemani nyuma Yako." Huko ni kusoma akili au telepathia ya akili ya aina gani?

55 Naye akasema, "Mimi nitakujilia." Sasa kumbukeni *Mimi*, *Mimi* alikuwa ni Mungu aliyetoa ile ahadi, Mtu yuyu huyu akasema, "Mimi." Na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. Vema. "Kwa muhula wake nitakujilia"

Ndipo Sara akacheka kimoyomoyo hemani, mwajua, "*Humph*!"

56 Ndipo yule Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Nyuma Yake. Sara akakana. Mungu angalimpiga papo hapo, bali asingeweza kwa sababu alikuwa sehemu ya Ibrahimu.

57 Dhambi zetu zingetuangamiza kama hatukuwa sehemu ya Kristo; Hawezi kulipiga Kanisa kwa sababu sisi ni wa Kristo. Mnaona? Sara na Ibrahimu walikuwa mmoja, Kristo na Kanisa Lake ni Mmoja. Dhambi zetu zimefunikwa na Damu Yake, kwa imani Yake, si yetu, tunatumainia kazi Zake zilizomalizika.

58 Sasa kumbukeni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu," vinginevyo, kujiliwa na kitu kile kile. Sasa, kama Mungu alionyesha ishara Yake mwishoni mwa Wayahudi, na mwishoni mwa kipindi cha wakati wa Samaria, na kuwaacha Mataifa waingie kwa theolojia ya kawaida tu, Yeye alikosea. Yeye hana kikomo, uamuzi Wake wa kwanza, jinsi ya kufanya chochote daima inabaki vile vile. Hapo ndipo tunapoamini Neno Lake, kwa sababu yale Yeye asemayo, Yeye hawezi kuyabadilisha.

59 Ninaweza kubadilisha yangu, kwa sababu nina kikomo; Yeye hana kikomo, wala hawezi kubadilisha Neno Lake. Kwa hiyo Mungu anaposema jambo lolote, weka nafsi yako juu yake, maana ni kweli. Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuwa na

imani, ni kuamini yale aliyosema, hivyo ndivyo tu unavyoweza kumpendeza, ni kuamini yale aliyosema.

60 Na hivi mliona, sasa hivi, kwenye saa ya mwisho, tulipoleta ambapo hili kongamano kuu la mwisho, ambapo Khrushchev pamoja na mataifa matano ya mashariki, kiongozi Eisenhower, mataifa matano ya magharibi yaliwakilishwa, na vile vidole kumi vya ile sanamu, hawatachanganyikana, naye Khrushchev akatoa kiatu chake na kukigongesha (Akili ya kiroho ingepata hilo upesi sana, mnaona.), kwenye dawati? Mnaona, hawatachanganyikana.

61 Jambo linalofuata ni kule kuja kwa lile Jiwe lililokatwa mlimani bila kazi ya mikono, ambalo litabingirika liingie kwenye ufalme wa Mataifa, utamalizika.

62 Kabla tu ya wakati huo, Yeye atamtuma Malaika huyu kwenye kanisa lipi? Kwa Sodoma? La. Kwa lile vuguvugu? La. Alilituma kwa Kanisa teule, lililoitwa litoke. Alionyesha ishara ya namna gani? Jambo lile lile alilofanya hapa jana usiku, Mungu, Elohimu akidhihirishwa katika Utu wa Roho Mtakatifu katika Kanisa Lake. Loo, jamani! Mbona, linapaswa kuturusha maili milioni moja angani kwa shangwe na sifa za utukufu Wake!

63 Mambo haya yalikuwa yakitukia hapo kabla tu, si yale maji kuanguka, Yeye alionyesha maadili ya watu, ambayo yangekuwa, lakini katika Sodoma, mnakumbuka, Yeye aliacha hilo, hilo linafasiriwa kiroho. Tuko katika wakati wa mwisho, enyi marafiki. Wazieni hilo usiku wa leo, na kama dhambi inaning'inia maishani mwako, wazia hilo.

64 Kesho, Mungu akipenda, nitawatuma hao wavulana huku, ama niwaambie kutoka papa hapa sasa wagawe kadi za maombi kesho jioni, yapata saa kumi na mbili, nafikiri. Hiyo karibu ni sawa, Ndugu Moore? Yapata saa kumi na mbili kesho jioni.

65 Sasa, wakati tukiwa hapa usiku wa leo, ombeni. Ni nani anayejua yale Mungu atakayofanya! Hatujui, Yeye ni Mungu. Na kama Mungu atafanya jambo moja, la kimbinguni, kuthibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa, thibitisho lisiloweza kukosea, basi jambo pekee likupasalo kufanya ni kusema, "Naam, Bwana, ninaliamini."

66 Afrika Kusini ambako makumi ya maelfu, mara maelfu walikuwa wameketi, ishara moja na watu ishirini na tano elfu kwenye viti vya magurudumu, vitanda vya wagonjwa, na machela, yaliokotwa malori saba makubwa ya mizigo wakati mmoja. Makafiri kwelikweli elfu thelathini wakavunja sanamu zao ardhini wakamjia Yesu Kristo.

67 Loo, jamani! Tumeshindiliwa sana na kila kitu, na kufadhaika sana na kuogopa. Msiogope. Hivi majuzi usiku nilihubiri juu ya jambo hilo, *Msiogope, Ni Mimi*. Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikuwa wakifa, wakizama, Shetani alikuwa akitaka kuwachukua, nao walidhani Yeye

alikuwa ni mzuka, roho, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia.

68 Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, Kitu pekee kinachoweza kukukomboa na kansa, Kitu pekee kinachoweza kukukomboa na ugonjwa wa moyo, dawa haina tiba kwa huo, Kitu pekee kinachoweza kukusaidia ni Kitu kile ambacho unakiogopa, unaogopa ni namna fulani ya roho, Ni Roho, Roho Mtakatifu, Kristo aliyedhihirishwa maishani mwetu. Mwaminini sasa.

69 Sasa, kesho usiku tutawaombea wagonjwa, na kesho asubuhi, Bwana akipenda, kama nitazungumza, sasa haya . . . mapenzi ya Bwana, nilitaka kuzungumza juu ya somo baada ya shule ya Jumapili: *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*.

70 Sasa, hebu na tufungue usiku wa leo kwenye Kitabu cha Yeremia, nami nitazungumza nanyi kwa muda mfupi tu juu ya, juu ya somo fulani. Hebu na tufungue Yeremia na tuanzie kwenye mlango wa 8 na kifungu cha 20 na hata pamoja na cha 22. Basi sikilizeni kwa makini hili somo, maneno yangu yatashindwa, Maneno ya Mungu hayawezi kushindwa. Mimi ni mwanadamu, maneno yangu hushindwa; Ya Mungu hayawezi, ni lazima yawe. Kifungu cha 20:

> *Mavuno yamekwisha, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka.*
>
> *Kwa sababu ya maumivu ya binti ya watu wangu nimeumia mimi; nimevaa kaniki; ushangao umenishika.*
>
> *Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu? mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

71 Na kama ningeliita somo, Ningetaka kuchukua maskini hayo, Neno tatu, Neno lenye herufi tatu, hasa: *Kwa Nini? Kwa Nini?* [Kiingereza: Why—Mfa.]

Na tuombe mara nyingine tena. Je, tunaweza? Kabla tu hatujalikaribia.

72 Baba, "Wewe ndiwe Kijito cha faraja yetu yote," kama vile kipofu Fanny Crosby alivyosema wakati mmoja, "zaidi ya uhai kwangu." Nasi tumeketi hapa usiku wa leo katika Maskani hii ya Uzima, maskani inayoitwa kwa jina la *Uzima*, si kwamba tu jina la nje *Maskani ya Uzima*, bali Bwana, watu walioko humu ndani, tuna Uzima wa Milele, kwa sababu tunakuamini Wewe, kwa maana imeandikwa katika Neno: "Yeye ayasikiaye Maneno yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

73 Jinsi tunavyoyapenda Maneno haya, kwa sababu Hayo ni Uzima kwetu. Neno Lako ni Uzima. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu."

74 Na imeandikwa vizuri sana tena katika Kitabu cha Waebrania na Paulo, tunaamini, mlango wa 4, kwamba "Neno la Mungu," ambalo ni Kristo, "lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, likikata hata kugawanya, hata kwenye mafuta ya mfupa, na," kiunganishi, "Mpambanuzi wa mawazo ya nia." Kwamba Neno, Neno ambalo ni Roho, Roho Mtakatifu, linaweza kuyatambua mawazo yaliyo niani mwetu. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili, Bwana!

75 Roho Mtakatifu pamoja na nguvu Zake za kuwaponya wagonjwa, na kuwaweka huru wafungwa, na kuwapa uhuru wote walio utumwani. Tunaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba utaikomboa kila nafsi kutoka utumwani.

76 Umchukue mwanamume au mwanamke ambaye ni mfuasi wa kanisa wala hakujui Wewe kama Mwokozi wao binafsi, jalia wakupokee Wewe usiku wa leo kama Mwokozi wao, warudi kanisani mwao kesho asubuhi, na kuishika mikono ya mchungaji wao, na kusema, "Mchungaji, nimekuwa mfuasi hapa kwa muda wa miaka *kadhaa*," ama miezi, ama chochote kile, "lakini jana usiku kweli niliusalimisha moyo wangu, mimi sasa ni Mkristo. Yesu ni Mwokozi wangu, nilimwona Yeye ni mtamu na mpendwa nafsini mwangu. Nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Nia yangu yote na malengo yangu ni tofauti sasa. Ninampenda, nami nitakuwa mshiriki bora wa kanisa hili kuliko nilivyopata kuwa hapo awali." Tujalie, Bwana.

77 Jalia wengi wajazwe na Roho Mtakatifu, wagonjwa waponywe, Mungu apokee utukufu. Tusaidie sasa tunapolitafakari hili neno kuu, swali, hasa, *Kwa nini?* Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

78 Sasa: *Kwa nini?* Hilo ni swali, wala hakuna mtu aliye na haki bora ya kuliuliza kuliko Mungu, Naye aliuliza hilo katika hili somo usiku wa leo. Kama Mungu akiwafanyia watu Wake njia ya kuepukia, kuepuka jambo baya sana, ama maradhi, ama mauti, ama, mauti ya Milele, na halafu watu wanashindwa kuipokea hiyo, Mungu huuliza, "Kwa nini? Kwa nini hamkufanya hivyo?"

79 Sasa, hilo litakuwa ni jambo kuu kwenye Siku ya Hukumu wakati Mungu atakapotuuliza sisi ambao tumekusanyika hapa usiku wa leo ambao hatutamkubali kama Mwokozi wetu na kujazwa na Roho Wake, "Kwa nini hamkufanya hivyo? *Kwa nini*?"

80 Nasi itatubidi kutoa jibu kwa hilo. Kumbukeni tu, tutawajibika kwa kila Neno ambalo Mungu ameandika. "Kwa nini hamkufanya hivyo? Kwa nini?" Wala hutakuwa na udhuru kwenye Siku hiyo, itatubidi kusimama mbele za Mungu.

81 Sasa, kama tu vile Mfalme wa Israeli hapo alipokuwa mwana wa Ahabu na Yezebeli, aliishi huko, huko Samaria, alikuwa ni mtu mwovu. Alikuwa kama baba yake, ama, mama yake, alimwabudu mungu wa mama yake, Baalimu. Basi siku moja

alipokuwa akitembea nje barazani, alianguka kupitia dirishani akaumia, akawa mgonjwa. Ndipo akawaita wawili wa watu wake wa miguu, askari akawatuma huko Ekroni na kuomba ushauri kwa manabii wa Baali, ama Baal-zebubu, hasa, endapo atapona au la.

82 Lakini unajua huwezi kumficha Mungu chochote. Huko chini kabisa nyikani mahali fulani kulikuwa na m—mhubiri mzee aliyemjua Mungu, jina lake lilikuwa ni Eliya. Mungu huwafunulia watumishi Wake siri Zake, naye Roho Mtakatifu akamjia Eliya, na kusema, “Kwea usimame njiani, na uwasimamishe.”

83 Ndipo Eliya akapanda upesi kilimani kwenye barabara iliyopitia mlimani hadi kwenye huo mji mwingine, naye akawasimamisha askari barabarani, na kusema, “Enendeni mkamwambie mfalme huyu kwamba hatoki kwenye kitanda hicho. Kwa nini? Kwa nini atume ujumbe kumwuliza Baal-zebubu kuhusu chochote? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Ni kwa sababu hakuna nabii huku chini? Je, ni kwa sababu Mungu hajajitambulisha Mwenyewe katika Israeli? Je, ni kwa sababu Mungu hajatoa nabii wa kumtaka shauri mambo haya? Basi kwa nini atume watu kule?” Alitaka kujua ni kwa nini.

84 Ndipo hao watu waliporudi, na kuleta ujumbe, Mfalme akasema, “Huyu alikuwa ni mtu wa aina gani?”

85 Akasema, “Alikuwa amejaa nywele, na alikuwa na kipande cha ngozi ya kondoo, ama amejifunga ngozi kiunoni mwake.” Basi mfalme akajua ya kwamba huyo alikuwa ni nabii Eliya, aliyekuwa na Neno la Bwana.

86 Haikuwa ni kwa sababu hakukuwako na Mungu katika Israeli. Haikuwa ni kwa sababu Mungu hakuwa na nabii wa kumtaka shauri, bali ilikuwa ni njia za ukaidi za Mfalme mwenyewe. Kamwe hakumpenda Eliya. Hakumpenda, kwa sababu Eliya sikuzote angemsahihisha katika dhambi zake, na nabii wa Mungu daima ni mkweli kwa Biblia. Haidhuru ni nini, yeye ana Neno la Mungu naye ni, anadumu moja kwa moja pamoja nalo. Nalo litamchochea mtu, na kama huyo mtu ni mwaminifu na mnyofu, atataka kurekebisha jambo hilo, lakini asipolirekebisha, basi anamgeuka huyo mjumbe, anajaribu kuizamisha hiyo Sauti.

87 Siku moja nilisoma makala katika gazeti moja huko Phoenix, nalo gazeti hilo lilisema kwamba kulikuwa na mtafuta madini aliyeuawa kwa sababu alikuwa na pesa na alikuwa akirudi, na m—mtu mmoja katili alikuwa akimfuata, naye mbwa wake akasimama apate kubweka, naye huyo mtu alikuwa akiota mchana kutwa jinsi atakavyozitumia hizi pesa akiwasili, naye akachukua bunduki yake, akaenda mlangoni na kumpiga risasi huyo mbwa.

Baadaye kidogo yule haramia akaingia, na kumwua huyo mtafuta madini, na kuchukua pesa zake; miaka mingi iliyopita. Nayo hayo yaliungamwa na huyo mtu kabla hajafa.

88 Mtafuta madini alifanya nini? Alikuwa amezama sana katika yale aliyokuwa akitaka kufanya na pesa zake, mpaka akachukua bunduki yake na kuinyamazisha sauti iliyokuwa ikijaribu kumwonya.

89 Hivyo ndivyo wanaume na wanawake wanavyofanya siku hizi. Wanatoka, labda wanajiunga na kanisa waone kama angalau halitawafariji kidogo, na kujaribu kuinyamazisha Sauti ya Mungu inayojaribu kuwaonya juu ya Hukumu ijayo. Wakijaribu kusema, "Mbona, ni ushupavu wa dini, ama ni kitu kingine." Kamwe hawatatulia muda mrefu kutosha kusikiliza. La, si kwa sababu hatuna Mungu, si kwa sababu Yeye hana wokovu kwa ajili yetu, ni kwa sababu hatutaki kumsikiliza.

90 Ni kama tu mtu anayeenda, ambaye atakufa, kwa ugonjwa wake, mlangoni pa daktari, huyo daktari anayo tiba ya kumpa huyo mtu kwa ajili ya ugonjwa wake, naye anaweza kumsaidia na dawa yake, lakini mtu huyo hataisikiliza, anakataa tu kunywa dawa ya daktari. Vema, mtu huyo angeweza kuwa karibu sana na daktari hata, angeketi mlangoni pake na afe, afe moja kwa moja kwenye kipandio cha ofisi yake, ama kuishi . . . majirani wake wa karibu, na kufa kwa ugonjwa ambao dawa ya kumtibu iko ofisini mwa huyo daktari.

91 Sasa, si kosa la huyo daktari, si kwa sababu hakuna dawa kule, ni kwa sababu huyo mtu anakataa kutumia hiyo tiba. Hiyo ni kweli. Anakufa kwa sababu anakataa kutumia tiba aliyo nayo daktari kwa ajili ya ugonjwa wake.

92 Ndivyo ilivyo kanisani siku hizi. Wanaume na wanawake wanafia kwenye marefu ya kanisa wakiwa dhambini, kwa sababu wanakataa tiba. Pana zeri katika Gileadi, huko kuna tabibu, lakini watu wanakataa kutumia hiyo tiba, hawaitaki.

93 Ni jambo la hatari kukataa dawa ya daktari. Kama una homa ya vipele vyekundu, au nimonia, chochote kile, na—naye daktari anakupa dawa, nawe unaimwaga tu, hilo ni jambo hatari, hiyo ni kweli, kwa sababu huenda ukafa.

94 Lakini ni hatari zaidi jinsi gani kuimwaga zeri ya Mungu, tiba ya Mungu! Kuidhihaki na kuiita ulokole, kumkufuru Roho Mtakatifu. Hakutakuwako na udhuru utakapoulizwa, "Kwa nini?" Ni jambo la hatari kufanya hivyo. Ni hatari kuupuuza mwili wako, vema, dawa iwapo daktari anayo kwa ajili ya ugonjwa wako, ni hatari zaidi kupuuza zeri kwa ajili ya nafsi yako, maana Mungu anayo.

95 Sasa, huwezi kuwasingizia na kusema, "Vema, si . . . ni kosa la daktari."

La.

"Hawana hiyo dawa."

96 Wanayo. Huwezi kusema . . . Si kosa la Mungu, ni kosa lako usipoipata. Ipo hapa kwa ajili yako, na mwaliko kwa yeyote atakaye, Mmethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri. Pentekoste si dhehebu, najua wanajaribu kuliundia dhehebu, bali huwezi. Pentekoste ni tukio linalowaendea Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki, "yeyote atakaye, na aje," mweusi, mweupe, wa manjano, wa hudhurungi, yeyote yule. Ni tiba ya Mungu, ndiyo zeri Yake kwa ajili ya dhambi. Pana zeri katika Gileadi, siku moja tutaulizwa ni kwa nini hatukuinywa.

97 Sasa, wakati mwingine katika kunywa dawa, wakati mwingine dawa si . . . Ni nzuri, Biblia inasema ni nzuri, "Moyo uliochangamka ni mzuri, kama dawa." Angalieni, lakini wakati mwingine dawa haitafanya kazi vivyo hivyo kwa huyo mtu, nawe huna budi kubahatisha hilo.

98 Nilishangaa hapa Afrika, kama huenda kuna daktari karibu, jinsi ambavyo Mungu huwashughulikia watu Wake. Mwenyeji mmoja aliniambia ya kwamba walipokuwa na kidonda ambacho hakingepona, wangeenda chini ya maskini mchungwa mwitu, na—na kuokota chungwa lililokuwa limejaa kuvu, kisha wakasugua kidonda hicho kwa hiyo kuvu. Penisilini. Waliijua mamia ya miaka iliyopita, nasi ndiyo kwanza tuipate hivi majuzi, halafu tunafikiri eti wao ni wajinga. Mungu huwashughulikia walio Wake. Kama tungetumia muda mwingi zaidi tukiomba, mambo mengi zaidi yangefanyika.

99 Sasa, tunaona ya kwamba wakati mwingine tunaweza kumpa mgonjwa penisilini kwa ajili ya nimonia, itaua kijidudu; halafu wakati mwingine tunampa mwingine, inamwua huyo mgonjwa. Huwezi kuwa na hakika sana nayo.

100 Nilikuwa nikizungumza wakati mmoja, nikitoa tamshi jinsi ambavyo dawa haikuponya, dawa ni msaada tu kwa maumbile. Nilipohojiwa kule Mayo, hivyo ndivyo walivyoniambia. Hebu ukate mkono wako, dawa haiponyi mkono wako, unautia dawa ipate kuuweka safi huku Mungu akiuponya. Mungu hujenga tishu, dawa haijengi tishu.

101 Kama ningeuvunja mkono wangu, na kusema, "Daktari, wewe ni mponyaji, uponye mkono wangu."

Angesema, "Bw. Branham, unahitaji uponyaji wa akili."

102 Hiyo ni kweli. Daktari anaweza kurudisha mkono wangu, hivyo ndivyo anavyofanya, anajifunza jinsi ya kuuunganisha, bali Mungu hana budi kuuponya. Hiyo ni kweli. Kwa sababu Yeye hutoa kalisi na uhai unaouunganisha mfupa huo, Mungu huuponya. Kwa hiyo, Zaburi 103:3 ilisema, "Mimi ni Bwana, akuponyaye magonjwa yako yote." Hiyo ni kweli. Ni Mungu. Mungu huponya kila . . .

103 Kamwe hapajakuwapo na dawa iliyoponya. Dawa yoyote inayoponya jeraha mkononi mwangu itaponya mtatuko katika koti langu, kama ambavyo nimesema mara nyingi.

Unasema, “Dawa haikutengenezewa koti lako, imetengenezewa mkono wako.”

104 Hebu nikate mkono wangu, nife papa hapa basi, wewe uushone mkono wangu, na kunishusha kwenye chumba cha maiti, na—na kuutia mwili wangu dawa uonekane wa kawaida kwa muda wa miaka hamsini, halafu unidunge sindano ya penisilini kila siku, na kuutia dawa, ndipo miaka hamsini tangu sasa kama mimi, mwili wangu ungali upo, lile jeraha lingekuwako, pia. Kwa nini isiuponye mwili wangu?

Unasema, “Uhai umetoka ndani yake.”

105 Basi kinachoponya ni kipi, dawa au uhai? Uhai. Hebu niambieni uhai ni nini, nami nitawaambia Mungu ni Nani. Mungu ni Uzima, Uzima wa Milele kuyasaidia maisha haya.

Mtu fulani akasema basi, “Vipi kuhusu penisilini? Hebu ujindunge penisilini.”

106 Nikasema, “Vema, penisilini ni kama tu sumu ya panya. Una nyumba iliyojaa panya wanaotoboa mashimo ndani ya nyumba, unamwaga sumu kidogo ya panya, inawaua hao panya, haizibi hayo mashimo. Penisilini huua kijidudu, bali Mungu hana budi kuponya seli ambazo zimeharibiwa nayo, kwa hiyo Mungu ndiye Mponyaji.” Ni sahihi.

107 Baadhi ya dawa zitafanya kazi kwa watu fulani, ambapo zitamwua mwingine, huwezi kuwa na hakika sana juu yake. Bali nataka kusema jambo moja: zeri ya Mungu ya dhambi humponya kila mtu, “yeyote atakaye.” Kuna, kama yeye ni, tabia yake, ama haidhuru ni nani, zeri ya Mungu ndiyo tiba ya dhambi, tiba maradufu. Naupenda ule wimbo wa kale tuliokuwa tukisema, “Iwe tiba maradufu kwa dhambi.” Napenda hilo.

108 Sasa, zeri ya Mungu, hakuna . . . si lazima uwe na wasiwasi juu ya hilo, hilo litajishughulikia lenyewe. Mara nyingi nimeshangaa, nami nina marafiki wengi wazuri madaktari, nao husoma majarida ya matibabu, na kadhalika, basi wakati mwingine ninapata moja la kusoma; ninapenda kuwazia jinsi Mungu anavyofanya katika weledi wa tiba.

109 Mnajua jinsi wanavyopata dawa? Vema, sayansi huchanganya kemikali mbalimbali pamoja, wanazijaribu, na baada ya kitambo kidogo wanapata fomula, nayo fomula hiyo, wa—wanamdunga nungubandia, huyo nungubandia akipona, wanakudunga wewe, waone inavyokufanyia. Wanaijaribu kwa nungubandia, na kama ikifaulu kwa nungubandia vizuri, basi wataijaribu kwa mwanadamu. Kwa hiyo wanadamu wote si kama nungubandia, kwa hiyo basi wanawaua wengine, wanaponya wengine.

110 Nimesikia ikisemwa kwamba, kwenye jarida, kwamba—kwamba ugonjwa wa moyo ulikuwa mwuaji namba moja nchini. Sio kuwa tofauti, lakini, sio kutokubaliana na watu hao waaminifu, lakini ningesema hivi: Ninatofautiana hivi, ugonjwa wa moyo sio mwuaji namba moja, dhambi-uaji ndiyo mwuaji namba moja, dhambi. Hiyo ndiyo inayoangamiza nafsi na mwili. Dhambi, mwuaji namba moja.

111 Nanyi mmesikia usemi wa kale, "Kamwe siwezi kujiepusha na kutenda dhambi, hakuna mtu anayeweza kujiepusha nayo. Sina budi kuvuta sigara. Inanibidi tu kunywa pombe mara kwa mara. Sina budi kufanya mambo haya." Mnajua ni kwa nini? Kwa sababu hawachukui tiba ya Mungu, chanjo Yake. Mungu ana dawa ambayo itakuchanja. Hiyo ni kweli.

112 Wanaiogopa. Wanahofu watafanya jambo lisilo la kawaida, wanahofu watatoka kwenye utaratibu wa kawaida, wanahofu kanisa halitakubaliana na yale wanayofanya, wanahofu majirani zao hawatakubali. Unamjali nini jirani yako, maadamu Mungu anakubali? Maadamu ujuzi wako unakubaliana na Neno la Mungu, vipi kuhusu hilo? Dumu na hilo.

113 Loo, ni kuzaliwa upya, wanaogopa hilo. Kuzaliwa upya ni kama kuzaliwa kokote kwingine, ni mchafuko. Sijali ni kuzaliwa kwa namna gani, ni mchafuko. Kama kuko kwenye zizi la nguruwe, ama kama kuko kwenye kitalu, ama kwenye chumba cha hospitali kilichopambwa waridi, ni mchafuko. Na vivyo hivyo kuzaliwa upya ni mchafuko, kutakufanya ufanye mambo ambayo hukuwazia ungeweza kufanya kamwe, lakini kutokana na mchafuko huo huja Uzima. Haleluya! Jambo ndilo hilo. Kutokana na mchafuko huja Uzima. Uhai hutokana na mchafuko.

114 Uhai hutokana na mauti, "Chembe ya ngano isipoanguka ardhini ikafa, hukaa peke yake." Lakini mradi inakufa na kuoza basi kutoka kwenye uchafu huo uliooza uhai huja. Mpaka mwanamume au mwanamke awe tayari kujifia wenyewe, kufa kwa kanuni zao za imani, kufa kwa mawazo yao wenyewe, na kutoka kwenye uchafu huo uliooza huja kuzaliwa upya kwa utukufu, na shangwe, na sifa za Mungu ambako kunamfanya atende tofauti, kunabadilisha tabia yake, kunabadilisha maisha yake, kunabadilisha nia yake, na kunabadilisha malengo yake.

115 Lakini wanakuogopa, wanaogopa kutawafanya walie na kuharibu vipodozi usoni mwao, wanawake; wanaogopa kutamharibia huyo mwanamume hamu ya sigara-nene. Mnaona? Wanakuogopa. Hawakutaki, wanaogopa mtu fulani atawaita watakatifu wanaojibingirisha ama—ama mlokole. "Kama wakimwita Bwana wa nyumba Beelzebuli, ni zaidi sana vipi watawaita wanafunzi Wake?" Hakika.

116 Kama hawakuniita hivyo, ningeshuka na kuomba, na kusema, "Bwana, nina shida gani?" Ulimwengu unawajua walio

wake, bali mmenunuliwa kwa gharama, "Ninyi ni watu tofauti, watu watakatifu, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu," nyinyi ni Ufalme.

117 Wakati fulani uliopita nilikuwa nikienda, mke wangu kwenye duka la vyakula nasi tukashangaa, hatukuwa tumeliona kwa muda mrefu sana, samahani, akina dada, kulikuwa na mama aliyevaa gauni. Hatukuwa tumeliona kwa muda mrefu sana. Nikasema, "Unajua nini? Mimi, kama ningalikuwa na kamera, ningempiga picha. Ninapaswa kwenda kumpa mkono."

Naye akasema, "Billy, ninataka kukuuliza jambo fulani, hao wanawake, baadhi yao huimba katika kwaya, wanaenda makanisani, nao wanasema ni sawa."

118 Nikasema, "Lakini Biblia ilisema ya kwamba mwanamke atakayevaa vazi, limpasalo mwanamume, ni chukizo machoni pa Mungu." Ndivyo alivyosema hasa.

Akasema, "Vema, kwa nini tunafanya hivyo na tunaamini hilo, sisi Wapentekoste?"

Nikasema, "Kwa sababu sisi si wa jamii yao, hatuko katika ufalme wao, sisi ni Ufalme tofauti."

"Loo," akasema, "Sisi ni Wamarekani, sivyo?"

Nikasema, "La." Nikasema, "Tunaishi Marekani, hiyo ni kweli, bali tumezaliwa."

119 Nilipoenda Finland, ndugu wote hushuka wanaenda, wanaingia kwenye bafu ya mvuke, moja ya mabafu ya Kifini. Kwa namna fulani nilijisikia vibaya, sikufanya hivyo. Dk. Manninen akasema, "Njoo, Ndugu Branham." Hakukuwa na sabuni wakati huo, mara baada ya vita.

Kasema, nikasema, "Asante. Si—siamini ninataka kufanya hivyo, sijui ni kwa nini." Ndugu Jack akicheka, kwa sababu alikuwepo.

120 Vema, hao ndugu wote walipanda kwenda kule wakaingia chumbani, wala sijui ni kwa nini sikutaka kufanya hivyo, bali niliketi tu huko nje. Huyu hapa anakuja maskini mwanamke mwenye nywele za rangi ya shaba pamoja na lundo kubwa la taulo, akiingia moja kwa moja kwenye kile chumba ambamo hao wanaume walikuwa wamevua nguo. Nikasema, "Hei, hei, hei! Simama!"

121 Akaangalia kote na kunipungia mkono, kisha akaingia ndani. Hawa hapa yapata dazani moja zaidi wanakuja, wakiwachukua hao wanaume huko nje na kuwaogesha. Baada ya hayo kumalizika, nikasema, "Dk. Manninen, hilo si sahihi."

Kasema, "Si zaidi ya wauguzi wenu wa Kimarekani wafanyavyo. Wamefunzwa tangu utotoni kuwa wanawake wa kusugua ngozi."

Nikasema, “Kwa vyovyote vile, si sawa.” Si sawa, Mungu aliwavalisha watu nguo, na kuwatenganisha kwa hizo. Si sawa.

122 Tukiingia Ujerumani, tunakuta watu wenye roho ya Kijerumani; Finland, tunaona watu wenye roho ya Kifini. Ilinishangaza nikiwa Sant’Angelo huko Rumi, kadiri huko kulivyo duni, kulikuwa na ubao kwa wanawake wa Kimarekani “Tafadhali vaeni nguo kwa heshima ya wafu.”

123 Awali ilikuwa Ufaransa iliyoongoza kwa mitindo, sasa tunaongoza. Wanakuja hapa kuona jinsi wanawake hawa wanavyovaa, wamewapita kwa mbali sana. Loo, ni aibu! Ni fedheha. Si kwa sababu Neno halijahubiriwa. Mungu ana mtu ambaye hatapatana na dhambi. Madaktari wapo, na zeri ipo. Ukimpokea Roho Mtakatifu, utavalia tofauti, utatenda tofauti, utakuwa tofauti, utaishi tofauti. Kwa sababu unakataa tiba, hivyo tu, unakataa tiba, unaogopa Kuzaliwa upya.

124 Mke wangu akasema, “Vema, sisi ni wa Ufalme wa aina gani?”

125 Nikasema, “Kila mtu katika milki yake mwenyewe, katika ufalme wake, anatenda hivyo, hao watu huko nje, Wajerumani wanatenda kama Wajerumani, Waswisi wanatenda kama Waswisi, Wafaransa wanatenda kama Wafaransa, na Wamarekani wanatenda kama Wamarekani.”

“Vema,” kasema, “kwani sisi si Wamarekani?”

126 Nikasema, “Kwa uwezekano, naam, tunaishi hapa, lakini tunapozaliwa kutoka Juu, tuna roho inayotoka mahali Patakatifu, ambako watu ni watakatifu na Mungu Mtakatifu, Mwokozi Mtakatifu, nanyi ni ukuhani wa kifalme, watu watakatifu, mmenunuliwa kwa gharama, mna hakika, wewe ni—wewe ni mgeni.”

Laiti ningaliweza kuimba wimbo huu wa kale:

> Sisi ni wasafiri na wageni hapa,
> Tunautafuta Mji ujao,
> Mashua Okozi inakuja hivi karibuni,
> Kukusanya Vito Nyumbani.

127 Loo, ninapenda hilo. Wasafiri! Ibrahimu, na Isaka, Yakobo alikuwa akiutafuta Mji ujao, wakikiri kwamba walikuwa ni wasafiri na wageni, bali walikuwa wakiutazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu, walikuwa wameonja mambo ya Mbinguni. Na mtu aliyezaliwa na Roho Mtakatifu si wa ulimwengu huu tena, anautafuta Mji na Ufalme ambamo utakatifu unatawala, ambamo Mungu anaishi. Kutafuta Mji ujao.

128 Waogopa kuzaliwa upya, kunakufanya tu mtu tofauti. Na endapo wewe si mtu tofauti, basi hujaongoka. Huenda ukaongoka katika dhehebu, huenda ukaongoka katika mazingira tofauti ama chochote kile, lakini unapoongoka

kwa Mungu, basi unaishi kitakatifu. Ninaamini katika utakatifu. Ninaweza kuwathibitishia kwa Biblia ya kwamba sijali ufanyalo, huwezi kumtolea Mungu sadaka kwa mikono michafu, Yeye hataipokea.

129 Matoleo katika Agano la Kale ilibidi yatakasiwe madhabahuni, kuhani, kabla hajaingia kuitoa, ilibidi atiwe mafuta na kutakaswa, la sivyo hiyo sadaka ilikataliwa. Mungu hataikubali sadaka kwa mikono michafu. Hiyo ni kweli. Haina budi kuja kupitia mikono mitakatifu, la sivyo Yeye hataikubali.

130 Wanaogopa kuzaliwa upya. Kwa sababu gani? Maana kwa namna fulani ni mchafuko kwao, bali kunaleta Uzima mpya, nina furaha sana.

131 Unajua kulikuwako na wakati ambapo hapakuwapo na dawa yoyote ya ndui duniani. Wengi walikufa kwa ndui, kwa sababu hakukuwako na dawa. Dondakoo, hakuna dawa, lakini sasa unaweza kupata chanjo yake. Janga linapotokea mjini, upesi, unashuka kwenda kupata chanjo ya ndui, ama sindano ya dondakoo, wanayo dawa. Ninashukuru kwa sababu ya hiyo, ninaifurahia, nina furaha tunayo. Na chanjo ya Salk kwa watoto wadogo, ninamshukuru Bwana kwa hiyo. Naomba ya kwamba atatupa zaidi na zaidi.

132 Ninaamini kama tukimchangamkia Mungu, kuna vitu hapa kwa ajili yetu, tuliumbwa kutoka duniani, mwajua. Kama tukimchangamkia tu, na kumwomba, na kuacha uovu wetu na kadhalika, mambo haya yote yangepatikana. Hiyo ni kweli. Lakini kwenu ninyi mnaoamini, Yeye anayo tiba zaidi ya hiyo. Hakika, anayo. Sasa, yote imetengenezwa, iko tayari kwa ajili yako.

133 Kulikuwa na wakati ambapo dawa, hakukuwako na yoyote, na watu wengi wakafa kutokana na magonjwa, lakini sasa unaweza kuchanjwa. Kulikuwa na wakati ambapo zeri ya Mungu haikuwa kamilifu, kwa sababu ilitolewa kwenye mishipa ya wanyama, nayo ilifunika tu dhambi, haikuiondosha. Lakini hakuna udhuru sasa, Mungu, siku moja, alifanya dawa.

134 Nitasema jambo fulani, Yeye hakuijaribu kwa nungubandia, alimpa Mwanawe. Alimchanja pale Yordani wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu Yake. Kila mtu, kila jicho lilimwangalia alipokuwa anaishi, aliishi maisha ya Mungu, alionekana kama Mungu, alitenda kama Mungu, aliishi kama Mungu, aliomba kama Mungu, aliponya kama Mungu, aliwafufua wafu kama Mungu, Yeye alikuwa Mungu. Mungu alikuwa, Yeye alikuwa—Yeye alichanjwa kutoka kwa mambo ya ulimwengu, nao wakamwangalia.

135 Katika saa ya kufa Kwake, hiyo chanjo ilishikilia. Wakati walipojua Yeye alikuwa ndiye yule Nabii, naye askari wa Kirumi akaweka tambara kichwani Mwake, na kufumba macho Yake, na kuchukua fimbo na kumpiga kichwani, na kusema, “Sasa, kama

wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini," chanjo ilishikilia.

136 Yeye hamjali ibilisi. "Ninafanya yale Baba anayonionyesha. Ninafanya tu yale Baba anayonionyesha kufanya." Ilithibitisha kwamba hiyo chanjo ilishikilia.

137 Wakati, basi, waliponyosha mkono na kuushika uso Wake, na kung'oa makonzi makubwa ya ndevu, wakatema mate makubwa ya ulevi na kuyaweka usoni Mwake, chanjo hiyo ilishikilia.

138 Wakati watoto Wake Mwenyewe walipoililia Damu Yake, hiyo chanjo ilishikilia. Yeye alisema nini? "Baba, wasamehe, hawajui watendalo."

139 Alipotukanwa, hakututukana, chanjo ilishikilia. Kuzimu yote ilikuwa ikiangalia kuona kama hiyo ingeshikilia. Alikuwa akitengeneza njia kwa ajili yangu na yako, akitoa mfano.

140 Wakati alipokufa msalabani, hiyo chanjo ilishikilia, na kwenye asubuhi ya Pasaka, haleluya, ilithibitika ndivyo ilivyokuwa. Ile chanjo, mauti yasingeweza kuizuia. Uzima na mauti haviwezi kuishi mahali pamoja. Alifufuka siku ya tatu, chanjo ikashikilia. Wakati akipaa Juu, watu walianza kuwa na shauku, walitaka hiyo chanjo, kwa kuwa hapo, hatimaye, kulikuwa na chanjo, kulikuwa na chanjo iliyotolewa na Mungu ambayo ingewafufua wafu kutoka kaburini, nao walitaka kuchanjwa.

141 Niliposikia habari zake kwa mara ya kwanza, niliitaka, pia. Nina furaha sana kwamba tungali tunayo kwa wingi, chanjo ya dhambi. Na wakati wote. . .Kulikuwa na mia na ishirini waliojifanya wagonjwa mara moja, kwa kuwa waliona ingeshikilia katika majaribu, "Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu, na mara Yeye angenitumia Mimi majeshi ishirini ya Malaika." Angeweza kufanya hivyo.

142 Lakini mnajua kama nilivyowahubiria hapa siku moja, *Mwana-Kondoo Na Hua*, Mnaukumbuka. Hua ananinii tu. . .alimwongoza mwana-kondoo, mwana-kondoo hawezi kujiongoza mwenyewe, hua alimwongoza. Naye mwana-kondoo ana kitu kimoja, hicho ni sufu, bali anapoteza hiyo, makusudi, kitu pekee alicho nacho.

143 Watu husema, mara nyingi wanawake huniambia, "Ndugu Branham, hiyo ni—hiyo ni haki yangu ya Marekani kama nikitaka kuvalia jinsi ninavyotaka kuvaa."

Hiyo ni kweli.

Wanaume wanasema, "Kama ninataka kunywa pombe ya kujifurahisha, wanaiuza huko nje, hakuna sheria dhidi yake, hiyo ni haki yangu ya Marekani."

144 Hiyo ni kweli, lakini kama Mkristo utapoteza haki zako za Kimarekani kama wewe ni mwana-kondoo; kama wewe ni mbuzi, hutazipoteza. Lakini kama wewe ni mwana-kondoo

utapoteza haki zako, kwa sababu wewe ni wa Ufalme mwingine, Hua anakuongoza.

145 Waliiona ikishikilia katika saa ya majaribu, ilishikilia katika saa ya kufa, na wakati alipokuwa kaburini siku tatu mchana na usiku, hiyo chanjo ilishikilia. Kwenye asubuhi ya Pasaka Malaika alilibingirisha na kuondoa lile jiwe, ndipo Mwana wa Mungu akafufuka tena, Naye akapaa Juu. Akasema, "Sasa, kama nyote mkitaka kuchanjwa, nendeni huko mkangojee katika mji wa Yerusalemu, nitatuma chanjo moja kwa moja kutoka Makao Makuu."

146 Loo, nina furaha sana! Loo, chanjo hiyo kuu, ungetoa nini kwa ajili yake, ingekuwa katika ofisi ya daktari usiku wa leo, ukishuka, na kusema, "Daktari, nidunge chanjo hii, na baada ya mimi kuishi maisha ya kawaida kisha nife, na hayo yote, muda si muda wajua asubuhi moja, nitafufuka tena kwenye Maisha mapya, na kamwe nisife kwa huo. Utanichanja, Dak"? Si ingegharimu kiasi cha pesa? Lakini ni bure usiku wa leo, si lazima uinunue, tayari imelipiwa. Pana zeri katika Gileadi. Loo! Samahani, mimi huchanganyikiwa ninapowazia jambo hilo.

147 Watu hawa, wanapochanjwa, wanatenda kiajabu. Kwa kawaida, wao hufanya hivyo wakati jambo kubwa linapotukia. Inawafanya kuwa wa kigeni wanapodungwa hii sindano. Ajabu yake ni kwamba wote walilewa, inaonekana, ama, wao walidhani hawa walikuwa wamelewa. Walikuwa wakicheza na kutenda kama kundi la walevi, nao—nao watu ambao hawakuchanjwa walisema, "Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya."

148 Wanaume na wanawake, sikiliza rafiki yangu Mkatoliki, bikira Mariamu alikuwa mle ndani, na kama bikira Mariamu, ma—mama wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ilimbidi kwenda hadi Pentekoste na kujazwa sana na chanjo ya Roho wa Mungu, hata akatenda kama mwanamke mlevi, utaingiaje, chochote pungufu ya hayo? Tafakari tu hilo. Utafanikiwaje? Haidhuru wewe ni wa kanisa gani. Yeye alikuwa mfuasi wa Kanisa Takatifu, pia, bali ilimbidi kupata chanjo, hicho ndicho kitu pekee kingefufuka, ilibidi Uhai uingie mle, alichanjwa.

149 Sasa, walipopata chanjo hii, walitoka wakaenda mitaani na kuanza ku—kufanya mambo ya kigeni sana, kucheza, kupiga mayowe, kukimbia huku na huku. Watu bila shaka walicheka, na kusema, "Wanaonekana kana kwamba wana kifafa." Lakini walikuwa wamepigwa chapa.

150 Ninakumbuka wakati nilipokuwa nikipanda farasi mbugani. Huko Colorado, tulikuwa na ng'ombe, Shirika la Hereford lililisha kwenye Bonde la Mto Troublesome. Kila majira ya kuchipua ilitubidi kuwaleta, kuwapiga chapa hawa ndama. Basi tulipoenda kuwapiga chapa hao ndama, wakati

mwingine wangekuwa ng'ombe wakubwa kidogo hapo kabla, wa mwaka mmoja, kabla hajapigwa chapa, labda.

151 Inawabidi kumwangusha chini, kuchukua chuma hiki cha moto cha kupiga chapa na kumwekelea, manyoya yangeungua, na loo, jamani, wakati alipomwachilia, alishikwa na mcharuko wa kutimua mbio, lakini ndugu, alikuwa ni wako, alikuwa amepigwa chapa. Ilimwumiza kidogo, lakini tulijua alikuwa wa nani baada ya hapo. Huenda ikadhuru kiburi chako, na kuchoma manyoya yako machache ya kikanisa, lakini utajua kuwa wewe ni wa wapi tangu wakati huo na kuendelea.

152 Chanjo, bila shaka. Walichanjwa, walikuwa wakifanya jambo fulani, wakaanza kunena kwa lugha zingine. Hao watu wakasema, "Sasa, haya yote yanamaanisha nini? Vema, tunawasikia hao watu, wote ni Wagalilaya, basi kwa nini tunawasikia wakinena kwa lugha yetu wenyewe, ambapo tulizaliwa? Hayo hayana budi kuwa ni matendo ya ajabu ya Mungu."

153 Ndipo basi kulikuwa na jamaa mdogo aliyesimama juu ya kisiki pale, akaanza kuwahubiria. Walikuwa na mengi ya... Walisema, "Tunaweza kupata chanjo hii? Tungependa kuipata hii. Tufanye nini tu—tupate kuchanjwa?"

154 Sasa, ile chanjo mpya ilikuwa ndiyo kwanza imwagwe, kwa hiyo walikuwa na zeri kwa wingi, nao walikuwa na daktari pale, jina lake lilikuwa Dk. Simoni Petro. Hilo linapaswa kuwafanya baadhi yenu makasisi kujisikia vizuri sana. Dk. Simoni Petro, yeye alizungumza juu ya hiyo chanjo.

Wakasema, "Tufanye nini tupate kuchanjwa?"

155 Akasema, "Nitawaandikia maagizo." Akasema, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtachanjwa." Hiyo ni kweli. Akasema, "Mbali na hayo yote, nitafanya haya ma—maagizo ya maisha, maagizo haya hayawezi kuchezewa tena. Mtu mwingine asijaribu kuandika moja kama hii. Shikeni agizo hili, kwa sababu ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Maagizo yale yale ni mazuri kwao, hiyo ndiyo chanjo.

156 Kama daktari akienda na kuandika maagizo, daktari mzuri kweli, anajua ni kiasi gani cha vitu fulani atakavyotia mle. Kimoja kinapaswa kuvuruga hicho kingine, kisipokivuruga, kama ukianza kuongeza vitu vingine mle ndani, ama kuongeza kitu kwake, ama kuondoa kitu kutoka kwake, utamwua mgonjwa wako. Bingwatapeli mwuza dawa akiongeza kitu kwake, ama kuondoa kitu kwake, huenda akamwua huyo mgonjwa.

157 Hiyo ndiyo shida ya mwenendo wetu wa kanisa siku hizi, sababu ya sisi kuwa na maskini makanisa mengi, yaliyokufa, wamejaribu kuchezacheza na agizo hilo. Ni agizo la Mungu.

Kuna zeri katika Gileadi, na huko kuna Tabibu. Usiyachezee hayo maagizo.

158 "Peana mikono na mtu fulani na kuwaingiza katika ushirika," hilo halihitaji toba. La, bwana. "Mnyunyizie mtu mtikiso wa chumvi uliojaa maji," haupachukui mahali pa ubatizo wa maji. Acha kuyachezea hayo maagizo! Pana zeri katika Gileadi, na huko kuna Tabibu.

159 Sasa, unangojea nini? Kwa nini ukatae agizo hilo? Daktari yupo hapa, Roho Mtakatifu, Yeye Ndiye aliyeandika hilo agizo. Walilitumia kote katika Agano, na kuendelea kwa miaka mia tatu au zaidi, hadi kwenye Baraza la Nikea. Ndipo wakaanza kuwaingiza watu mle ndani, na kuanza kuingilia *hapa*, na kunyunyizia, na kumwagilia, na namna zingine zote na kadhalika. Lakini rudini kwenye lile agizo la asili! *Hilo hapo* lile agizo. Sababu ya watu kujaa dhambi hivi, hawachukui maagizo ya Mungu. Wanajiunga na kanisa badala ya kuzaliwa ndani Yake. Wanajaribu kuchukua kitu kingine mbali na Matendo 2:38, hayo ni maagizo ya Mungu.

"Je, hakuna zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?"

Naam, pana zeri katika Gileadi. Naam, kuna matabibu kule, wengi wao. Hakika. Nawaambia ukweli juu yake.

160 "Basi mbona binti ya watu Wangu," yule binti, maskini kanisa siku hizi, u—unabii unaendea wakati huu, "mbona binti ya watu Wangu basi, binti ya watu Wangu," ambaye alikuwa huko nyuma kwenye mwanzo, ambaye anatumia agizo lili hili, "mbona binti ya watu Wangu angali ni mgonjwa? Kwa nini? Hivi hakuna mtu wa kuwaambia ukweli?"

Hakika.

"Je, hakuna zeri huko, bado ni Roho Mtakatifu?"

Kuna mamia walioketi papa hapa usiku wa leo wanaoweza kuthibitisha kwamba Roho Mtakatifu ni wa kweli. Hakika, wapo.

161 Basi, ndugu, kama hujapata kuchanjwa dhidi ya dhambi bado, chukua maagizo ya Mungu, na kuna zeri katika Gileadi, na huko kuna Tabibu, kuna tangi la maji kwenye orofa ya chini, na madhabahu hapa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

162 Bwana, Wewe umekuwa Mungu wa kale, Wewe ni Mungu wala hubadiliki, kama ukiwahi kuandika maagizo, Ewe Tabibu mkuu, hayawezi kubadilishwa. Tunakumbuka yale maagizo uliyoandika Wewe, yalisema:

> *Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka;. . .asiyeamini, atahukumiwa.*

*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Kwa jina langu watatoa pepo;. . .watasema kwa lugha mpya;*

*. . .wakishika nyoka;* ama *wakinywa. . .kitu cha kufisha, hakitawadhuru;* wakiweka. . .*mikono* yao *juu ya wagonjwa,. . .watapata afya.*

163 Maneno Yako ya mwisho kwa Kanisa Lako. Mara baada ya hayo, ulinena kupitia mtume Petro, katika umbo la Roho Mtakatifu wakati alipomwagwa mara ya kwanza. Nilimwita daktari usiku wa leo, Bwana, ili tu kutoa ho—hoja, ilikuwa ni Roho Mtakatifu, uvuvio, ujuzi ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ameandika fomula hiyo, nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

164 Kunao watu hapa, na labda, katika wasikilizaji wetu ambao kamwe hawajaikubali fomula hii. Huenda wakawa ni wafuasi wa kanisa, ama kitu fulani, lakini kuhusu kumpokea Roho Mtakatifu na kuchanjwa, Roho mle ndani anayeiondoa tabia yao ya kale, anaiingiza ile asili mpya, hawajampokea bado. Ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba usiku wa leo, kwamba watampokea, kwamba wenye dhambi watakuja Kwako, nao watakupokea Wewe kama Mwokozi wao binafsi, wajazwe na Roho Mtakatifu. Jalia, Bwana, kwamba wale wanaoingia majini, hakuna hata mmoja wao atakayeingia majini usiku wa leo bila kutoka na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

165 Jalia huu uwe usiku wa ukumbusho, ambao utakumbukwa kwa muda mrefu, kwa sababu ya Uwepo Wako, na Wewe, Daktari Mkuu, hapa kufanya kila kitu ulichoahidi: kuwapa Uzima wale wanaokufa, kuponya maradhi kwa wale ambao madaktari wetu wapendwa hawawezi kuyagusa: moyo, kansa, vipofu, viziwi, bubu, waliopooza, kitu ambacho Wewe hujaweka mioyoni mwao bado, ama katika nia zao, kitu cha kuondoa hayo, labda hakuna kilichosalia ila Damu tu. Lakini tunajua, Bwana, ya kwamba chanjo hiyo hapo huponya yote. Tunakushukuru kwa ajili Yake, Baba. Twaomba sasa kwamba Wewe utapata utukufu kutokana na ibada hii. Tunaomba hayo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nampenda, nampenda
. . .alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

166 Hivi Injili ya mtindo wa kale haiwasugui tu? Mnajisikia safi? Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu, kwa uchaji. Sasa hebu na tuuimbe polepole na kwa upole sasa, tukiwa na ibada mioyoni mwetu kwa Mungu.

Nampenda. . .-mpenda
Kwani alipenda kwanza. . .
Na. . .wokovu
Mtini Kalvari.

167 Hebu tuuvumishe tu. Sijui, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, huku muziki ukipigwa kwa utamu, hao wasichana, kama wataupiga, kunaweza kuwako katika uwepo wa Kiungu, mwenye dhambi fulani ambaye angesema, “Ninataka kumpenda, Ndugu Branham, kweli ninataka. Daima nimetaka kufanya hivyo. Laiti ningalikuwa na ujasiri, usiku wa leo, kumpokea kama Mwokozi wangu binafsi”? Waweza tu kuinua kichwa chako, ama mkono, hasa, wakati hakuna mtu anayeangalia? Juu kabisa kwenye roshani, huko nyuma kabisa, ninaamini ninawaona watu weusi huko nyuma, kwenye orofa ya juu kabisa. Inua mkono wako sasa. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

Mungu akubariki. Ninauona mkono wako. Mungu akubariki. Hiyo ni . . .

168 “Loo, Ndugu Branham, laiti ningalikuwa na hakika ya kwamba Yesu yupo hapa! Ninaamini ulisema kweli, ninaamini Yeye kweli alisema hilo, ‘Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.’ Unatwambia ya kwamba, tuko—tuko kwenye mwisho wa safari.”

Nyuma hapa sehemu hii ya mkono wangu wa kulia, inueni mikono yenu. Hiyo . . . Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Huko nyuma kabisa. Hilo ni zuri.

169 “Ninaamini, Ndugu Branham, ya kwamba ni kweli, hata hivyo sijawahi kuwa na kitu chochote ambacho ningeweza kuweka mikono yangu juu yake kusema ni cha kimbinguni. Nimesikia jumbe kuu kwenye Biblia, bali kamwe sikumwona Roho Mtakatifu akija na kufanya lolote. Na, hasa, ulipokuwa ukizungumza usiku wa leo, kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, Naye akaonyesha ishara ya Masihi, nawe ulisema aliionyesha kizazi hiki, Naye aliahidi angefanya hilo kama ilivyokuwa katika siku zile kabla ya kuteketezwa kwa dunia huko Sodoma, Yeye angeonyesha ishara iyo hiyo, angefanya kazi katika mwili wa mwanadamu na kufanya jambo lilo hilo kabla tu ya kuteketezwa kwa dunia, kama ningeweza kumwona Yeye, kitu ambacho ningeweza kuweka mikono yangu juu yake kujua ya kwamba—ya kwamba Kristo yuko papa hapa, ningempokea kama Mwokozi wangu binafsi.”

170 Huenda kukawa na mwingine ambaye hawajainua mikono yao? Inueni mikono yenu. Siwezi kuona vizuri sana kwenye roshani, huko juu kabisa. Inaonekana kama, naam, ninaiona hiyo mikono, watu weusi. Mungu awabariki huko juu, naam. Chini kwenye orofa za chini hapa mahali popote, mnaosimama kwenye viti vya juu huko nyuma, huko nyuma kwenye, huko sehemu zote za nyuma mahali fulani, mahali popote. Mungu akubariki hapa, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, maskini ewe mtu. Ubarikiwe. Vema.

171 Baba yetu wa Mbinguni, sasa kwa kuwa wakati umewadia ambapo nimenena habari Zako, nikielezea ya kwamba Wewe ndiwe Tabibu Mkuu na una nguvu za chanjo kufanya mambo, kwamba Wewe hujafa, kwamba Wewe ulikufa, kweli, bali ulifufuka tena siku ya tatu, Nawe u hai milele. Nawe uliamuru, ama ululiagiza Kanisa Lako liende ulimwenguni mwote, na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe kitakachoamini, naye aliyeamini na kubatizwa, angeokoka. Nawe ulisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya."

172 Na jinsi ulivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi na Wasamaria, sasa, Bwana, kanisa la Mataifa limekuwa na miaka elfu mbili ya theolojia, kamwe hawakuona jambo hilo mpaka wakati huu. Nabii alisema, "Itakuwa Nuru jioni." Tunajua ya kwamba jua huchomoza, kijiografia, mashariki na kutua magharibi. Jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi.

173 Nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa mchana wala usiku, siku yenye utusitusi," Nuru ya kutosha tu kujiunga na kanisa, na mambo machache kama hayo, "lakini wakati wa jioni, Nuru za jioni zingeangaza."

174 Uliwatokea watu wa mashariki kwa Wayahudi, Wasamaria, ukawaangazia Nuru hiyo. Sasa tumekuwa na miaka hii mirefu elfu mbili, siku ya vita vya majonzi na matatizo, lakini Nuru za jioni zimeanza kuangaza, Mwana yeye yule wa Mungu pamoja na nguvu Zake zile zile, akionyesha ishara zile zile Zake, kama tu vile jua linavyoshuka kwenye upeo wa macho wa magharibi. Hatuwezi kuendelea mbele zaidi, Bwana, tuko kwenye Pwani ya Magharibi, ingekuwa ni kurudi mashariki tena. Bwana, tuangazie usiku wa leo, utuonyeshe Uwepo Wako iwapo inakupendeza.

175 Ninaomba ya kwamba utamjalia yule Mjumbe wa Agano aliyekutana na Ibrahimu pale kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma, wakati alipokuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na Roho aliyekuwa ndani Yake, Ambaye Ibrahimu alimtambua kuwa Mungu Mwenyezi, yule El mkuu, Elah, Elohimu, Yule anayeishi Peke Yake, aliyedhihirishwa katika mwili wa nyama ambaye alikula ndama wa ng'ombe, akala siagi, na maziwa, na ugali wa mahindi, kisha akatoweka moja kwa moja machoni pa Ibrahimu, Elohimu.

176 Wakati alipodhihirishwa katika mwili kwa kuzaliwa na bikira, akaahidi ya kwamba katika siku za mwisho ishara hii ingetendeka kabla tu hajawarudia Mataifa. Sisi hapa, Bwana, Wewe hutimiza Neno Lako. Nimewaambia watu hawa kwamba wao ni, waliokolewa wakati Yesu alipokufa kwa ajili yao, waliponywa wakati Yesu alipokufa kwa ajili yao, thibitisha Neno Lako. Kama tu utafanya hivyo usiku wa leo, Bwana, hawa watu watatambua ya kwamba Wewe upo hapa.

177 Usingeweza kuwaponya, kwa sababu tayari umefanya hivyo, kilichobaki ni imani yao kuudhihirisha. Je, utakuja usiku wa leo, Bwana, na kuthibitisha Uwepo Wako, kama sisi, watumishi Wako wanyenyekevu, tumepata neema machoni Pako?

178 Kama ungenitia mafuta, mtumishi Wako, Bwana, ingekubidi kuwatia mafuta wasikilizaji Wako, pia, kwa sababu haina budi kupitia kwa wote wawili. Kwa kuwa tunatambua ya kwamba ulipokuwa hapa duniani, ulipowaendea watu Wako Mwenyewe, ilisema, "Hakuweza kufanya kazi nyingi kuu, kwa sababu ya kutokuamini kwao." Ndivyo ilivyo usiku wa leo.

179 Sikia, Baba, tunajikabidhi Kwako, na kungojea kwa unyenyekevu kwamba utadhihirisha neema Yako na upendo kwetu, ndipo tutawaomba wenye dhambi waje mbele kupokea maagizo. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

180 Mbele za Mungu, Malaika watakatifu, ninasema nitasonga mbele katika Roho kumpa changamoto adui asiyeonekana miongoni mwetu, huyo ni maradhi, magonjwa, hayo ni pepo, kama kansa. *Kansa* ni neno la kitabibu, nafikiri *kaa*, mwajua, yule mnyama wa baharini, miguu, bali ana uhai. Kansa ni seli, seli mwitu, ninavyofahamu mimi, mimi si daktari, bali ni uzidishaji wa seli. Vivyo hivyo wewe nawe ni uzidishaji wa seli, uhai wako ulikuja kupitia ndoa takatifu, kwa mapenzi ya Mungu. Lakini kansa hii ilitoka wapi? Kuchukua maisha yako. Yeye ni ibilisi.

181 Yesu alisema wakati pepo bubu na kiziwi alipomtoka huyo mtu, pepo bubu na kiziwi, angeweza kuongea. Mnaona? Roho.

182 Maskini ndugu huyo huenda alienda kwa daktari mzuri, naye akamchunguza, akasema, "Naam, bwana, nimeipata. Una mshipa uliokufa sikioni mwako, na huo ndio unaokufanya kiziwi."

183 Sasa, kwa nini hakuwa amekufa, akiwa na mishipa mwili mzima? Mnaona? Ni kama nguvu zisizoonekana zikimnasa. Kitu ambacho daktari anaweza kufanyia kazi, anaweza kuona, kwa—kwa mikono yake. Ana hisi mbili anazotumia, hizo ni kile anachoweza kuona kwa macho yake, kile anachoweza kugusa kwa mikono yake. Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia ndizo zile hisi tano za mwili.

184 Sasa, kama angaliweza kukiona, angeweza kukishughulikia, bali kuona kitu hiki kilichoua huo mshipa hawezi kukiona, kama utepe wazi, ama chochote kile. Sasa, ni roho kiziwi, hebu itoe hiyo hapo, maumbile hakika yatazunguka yenyewe.

185 Ni kama tu shina la mahindi, ua hili linapokua, kama likiwekwa juu ya bonge la udongo, na limesongonyoa, ondoa tu hilo bonge, litakua tena moja kwa moja. Huna budi kuwa na . . . Huna budi kutafuta vyanzo kabla hujapata tiba.

186 Ukiingia kwenye ofisi ya daktari, na kumwambia, "Ninaumwa na tumbo langu," naye anakupa aspirini, akakurudisha nyumbani, ama ana shughuli nyingi sana asiweze kujipumbaza nawe, au hajali. Daktari mzuri atakukaribisha ndani, inakugharimu zaidi kidogo, bali atakuchunguza mpaka apate chanzo chake, na halafu aanze kufanya kazi hapo.

187 Sasa, si kama daktari wa tiba, bali kama mtumishi wa Kristo, ninajua chanzo chake, ni dhambi. *Dhambi* ni nini?

"Ndugu Branham, sitendi dhambi."

188 Kutokuamini ni dhambi. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Kutokuamini ndiyo dhambi pekee iliyopo. "Yeye asiyeamini amehukumiwa." Wewe. . .Kusema uongo, kuiba, kufanya uzinzi, hiyo si dhambi, hizo ni sifa za kutokuamini, hiyo ni kweli, sifa za kutokuamini. Kama uliamini, usingefanya mambo hayo.

189 Sasa, Roho Mtakatifu aliahidi kuja katika siku za mwisho na kuonyesha jamii ya Mataifa ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, kwamba ingekuwa Mungu juu yetu, katika Ubaba; Mungu pamoja nasi, katika Uwana; sasa Mungu Roho Mtakatifu ndani yetu, mnajua hilo. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata mwisho wa ukomo." Ni, Yeye atakuwako muda gani? Mpaka mwisho, ulimwengu ukiisha, Yeye angali atakuwa ndani yako, Mungu ndani yako.

190 Sasa, kama Roho Mtakatifu. . .Huyu ndiye Roho Mtakatifu, Malaika huyu wa Mungu ambaye wao, sayansi ilimpiga picha, imetundikwa huko Washington, DC, yenye hatimiliki, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha. Ninawaambia katika Jina la Kristo: Hayuko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu ninasema yale ninayosema, Yeye yupo hapa.

191 Hakuna mtu ninayemwangalia katika jengo hili ninayemjua. Naam, ninaamini. Ninamjua huyu Ndugu Ed Daulton, ndugu huyu mhubiri wa Kibaptisti, aliyeketi papa hapa kutoka huko juu Kentucky, na hao wavulana wawili walioketi karibu naye. Nje ya hao sioni hata nafsi moja niijuayo.

192 Ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa na wanamhitaji Kristo kwa ajili ya uponyaji wako, wa kimwili, ama kwa ajili ya mpendwa fulani, ama kitu fulani unachohitaji kwa Kristo, nawe unajua sikujui, sijui unachotaka? Inua mkono wako. Amini, vema, amini tu. Kisha, katika imani yako, mwamini Mungu kwa moyo wako wote.

193 Sasa, iweni na kicho kabisa. Halafu basi, sasa, chukueni tu muda wenu, kwa dakika moja tu, msiwe na wasiwasi, basi wakati mnapoamini hilo, na kuninii. . .Nitanukuu Andiko kutoka katika Kitabu cha Waebrania mara tu nitakaponukuu hili.

194 Yesu wa Nazareti, Bwana na Mwokozi wetu alikuwa akienda Zake kumfufua maskini msichana mdogo wa kuhani aliyefariki, na kulikuwa na mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu. Alikuwa amejaribu kuponywa kupitia kwa waganga, nao walikuwa wamejaribu sana kumponya huyo mwanamke, bali wasingeweza kumponya. Alikuwa akitokwa na damu, labda kukoma hedhi, ama chochote kile, isingeweza kukoma, nami ninaweza kuona maskini huyo aliyekwajuka, akasema moyoni mwake, "Kama nikiweza tu kugusa vazi la Mtu huyo, nitakuwa mzima." Mnakumbuka hiyo hadithi.

Naye akaligusa vazi Lake, na Yeye akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

Ndipo Petro akamkemea, akisema, "Kila mtu anakugusa. Kwa nini ukasema jambo kama hilo?"

Akasema, "Lakini nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka," uweza.

195 Sasa, unasema, "Loo, mimi ni mgonjwa usiku wa leo, Ndugu Branham. Kama Yesu angalikuwa hapa, ningemgusa sasa hivi."

Ungefanya hivyo? Hakika, ungefanya. Vema, ninataka kukwambia Yeye yupo hapa. Um-hum, vema. Mnaona?

Sasa, kama Yeye—Yeye angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, kama ungemwendea, na kusema, "Bwana Yesu, utaniponya?"

Angesema, "Tayari nimekuponya. Unaamini?" Hapo ndipo, "Na iwe kwako sawasawa na imani yako," Yeye alisema. Mnaona?

196 Ilikuwa tayari imekwisha wakati alipokufa pale Kalvari, bali Yeye anaweza kujifanya Mwenyewe kuwa hapa kuonyesha ya kwamba yu hai wala hajafa, aliahidi hilo, hiyo ndiyo faraja yetu. Hivi hamna furaha katika saa hizi zenye giza, wakati ulimwengu, ama, na, hakuna mtu anayejua la kufanya, hata hivyo tunajua mahali tunaposimama? Tunajua. Mnaona? Yuko hapa. Tunamwamini, Huyu hapa, na imethibitishwa kisayansi ya kwamba Yeye yupo hapa, kwa picha zao, na kadhalika. Kanisa katika mamilioni kote ulimwenguni linaona nguvu Zake, linaziona zikifanya kazi.

197 Na kuna, kumbukeni, kuna jambo fulani kuu ambalo liko karibu kutukia, saa haijafika bado, jambo fulani litatukia, nanyi mtajua moja ya siku hizi, muda si mrefu sasa. Usiache iwe imechelewa sana, kumbukeni, mara nyingi mambo haya hupita, wala hamjui.

198 Kanisa Katoliki halikujua wakati walipomteketeza Joan wa Arc kama mchawi ya kwamba alikuwa mtakatifu; hawakumjua Mtakatifu Patrick vivyo hivyo; hawakujua Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu mpaka alipokuwa amekufa, akazikwa, na kufufuka tena, wakatambua yale waliyokuwa wamefanya.

Usimkatae huyu Roho Mtakatifu, kwa kuwa siku moja utatambua yale umefanya. Unaona? Usiache iwe hivyo.

199 Sasa, Yeye yupo hapa, na Biblia inasema ukitaka kumgusa, Waebrania, yeyote wa makasisi hapa anajua hili, Biblia inasema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu aliyeketi mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Je, Waebrania 13:8 inasema ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ungemgusa, Yeye angetenda vile vile. Hiyo ni kweli? Jambo lile lile alilofanya kule chini wakati yule mwanamke alipomgusa, Yeye angefanya jambo lile lile, kwa sababu Yeye aliahidi angefanya hivyo, kulingana na yale aliyofanya pale alipokuwa akizungumza na Ibrahimu. Mnaona?

200 Kama unaamini kwa moyo wako wote, Roho Mtakatifu na aje, kwa karama ya Kiungu. . . Sina kitu ndani yangu, kama tu maikrofoni hii, ni bubu isipokuwa, ni bubu bila kitu kinachopiga kelele upande huu wake. Vivyo hivyo mimi ni bubu kabisa, bila Kitu fulani kunena kupitia kwangu; sikujui wewe. Mguse Yeye, na unapofanya hivyo, unawasha kitu kinachomshusha Roho Mtakatifu chini.

201 Kama ninaweza kujiachilia, na kujinyenyekeza kuyaondoa mawazo yangu njiani, imani yako katika Mungu itamgeuza, Naye atamtumia Roho Wake Mtakatifu ndani yangu kufanya jambo lile lile alilomfanyia yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. Haitakubidi kuwa na kadi yako ya maombi, na kuja huku juu, maana hamna kadi zozote za maombi, kwa vyovyote vile. Mnaona? Tutazigawa kesho. Iweni tu na imani.

202 Sasa sikilizeni, mtu yeyote asisumbue, asipige kelele, aminini tu, na muombe sasa kwa dakika moja, ninapogeuza mgongo wangu, muone kama tuko kwenye mwisho wa safari.

203 Mungu, ni kwa heshima na utukufu Wako, tunaomba. Mwenyezi na Mungu mwaminifu sana, Ambaye hutimiza Neno Lako katika kila kizazi, bila kushindwa, bali daima upo kujithibitisha Mwenyewe kuwa hai, siku moja wakirudi nyumbani kutoka kwenye ule ufufuo, wengi hawakukuamini Wewe, na kulikuwa na mmoja jina lake Kleopa, naye na rafiki yake walikuwa wakienda zao Emau. Nao walipotembea pamoja Nawe siku nzima, na ulikuwa umezungumza nao, hata hivyo hawakukutambua Wewe, mpaka ulipowafikisha chumbani, wamejifungia ndani.

204 Kuna wengi hapa usiku wa leo, Bwana, ambao wametembea pamoja na Wewe miaka hii yote, na wangali hawatambui jinsi ulivyowaepusha na ajali, na mambo mbalimbali yaliyotukia, na ukawajalia kuwa hai wapate kuwa hapa usiku wa leo. Na wakati tukiwa tumefungiwa ndani kama vile Kleopa na rafiki yake walivyokuwa, fanya jambo kama Wewe ulivyofanya wakati huo. Wakati ulipofanya jambo fulani kama tu ulivyolifanya

kabla hujasulubiwa, walijua ya kwamba Wewe ulikuwa Yesu yeye yule, kwa kuwa hakuna mtu aliyelifanya hivyo ila Wewe. Nao wakakimbia upesi, na kuwapasha wengine habari, "Hakika Bwana amefufuka."

205 Sasa, Baba, fanya usiku wa leo katika kusanyiko hili kama ulivyofanya katika siku ulipokuwa hapa duniani, kwa sababu inalingana kabisa na ahadi Yako. Nena, Ee Mungu, tunapojinyenyekeza na kuyakabidhi maisha yetu mkononi Mwako. Laiti ungalilifanya mara moja tu, Bwana, mara moja zaidi, ndipo watu hapa wataulizwa sababu mbona hawakufuata maagizo ya Biblia, kwa kuwa wanaona ya kwamba, kweli, Mungu anatenda kazi kupitia Kanisa Lake na kupitia watu Wake. Jalia kwa unyenyekevu niombe jambo hili, Mwokozi wetu mwenye fadhili, na mwenye upendo, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

Vema, inueni vichwa vyenu.

206 Ninaangalia moja kwa moja huku chini kwa mwanamke ambaye ameinua kichwa chake akiomba. Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini moja kwa moja huko juu Nuru ile imening'inia, ile Nguzo ya Moto, nami ninaiangalia wakati ikitenda kazi. Huyo mwanamke alikuwa akiomba nigeuke na kumwita, naye, anaugua ugonjwa wa rektamu. Kama ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa.

207 Maskini mama huyo anatoka, huenda mnajua ni nani, anatoka Fort Smith, Arkansas. Simama kwa miguu yako, maskini mama, uliye na shali ndogo mgongoni mwako huko nyuma, ugonjwa wako wa rektamu umekuacha, unaoitwa bawasiri.

208 Sasa, ninainua mikono yangu kwa uchaji, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, kumjua. Mimi. . .Huna kadi ya maombi, sivyo? Kwa sababu hakuna kadi za maombi. Sikujui. Ni, hiyo ni kweli? Hatufahamiani. Inua mkono wako, ili watu wapate kuona. Mimi kamwe. . .Je, yale aliyowaambia, yalikuwa ni kweli? Punga mkono wako, kama ni kweli.

209 Ninataka kuliuliza kusanyiko jambo fulani: Huyo mwanamke alimgusa nani? Anainua mikono yake, hajawahi kuniona, wala sijawahi kumwona. Na hata hivyo Roho wa Mungu yuko hapa kumrudia, Yeye yule; alikuwa na imani kama yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake. Kamwe hakunigusa, angalieni jinsi alivyo mbali nami, alimgusa Kuhani Mkuu. Hilo linathibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa.

210 Mama aliyeketi moja kwa moja nyuma pale mwisho, hiyo kofia ndogo yenye manyoya, anaomba, pia. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaugua mgongoni mwako kutokana na ajali, ajali ya barabarani. Hiyo ni kweli. Mbali na hayo una yabisi kavu, hiyo ni kweli, matatizo. Una mpendwa unayemwombea,

mwana, ugonjwa wa wasiwasi. Una mume unayemwombea, yeye ni mlevi sugu. Hiyo ni BWANA MUNGU ASEMA HIVI.

211 Je, unamkubali Yesu Kristo sasa? Kama mambo hayo ni kweli, inua mkono wako, kusudi watu waone. Endapo sikujui, nawe hunijui, punga mikono yako. Sina njia . . . Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Basi nenda ukapokee ulichoomba, unaweza kukipokea.

"Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana kwake aaminiye." Kama unaamini, inakubidi kuamini kwanza.

212 Hebu tuone sasa. Mnaona, mimi, njia pekee nitakayopata kujua yale niliyomwambia mwanamke huyo, ni kwenye kanda. Huyo hakuwa ni mimi nikizungumza, huyo alikuwa ni Yeye, bali kuna Kitu fulani ambacho bado kinamshikilia huyo mwanamke.

213 Anashangaa, loo, ni—ni nanii wake, nanii, m—m—m—mvulana, wasiwasi, la, mimi, hili hapa, ni pepo mchafu aliyemfanya huyu mvulana ashikwe na fadhaa, na iko juu ya jamaa huyu hapa. Amevurugikiwa, pia, ametoka Georgia, yeye ni mhudumu. Kasisi Farrell, kuvurugika kwako kumekwisha, bwana, wasiwasi wako umekwisha. Yesu Kristo anakuponya.

Sasa, kwa huyu—kwa mtu huyu, sijawahi kumwona maishani mwangu, hatufahamiani kabisa. Mwulizeni.

Je, mambo hayo yalikuwa ni kweli, bwana? Punga mkono wako kama hiyo ni kweli. Je, yale aliyokwambia yalikuwa ni kweli? Sikujui. La, bwana.

Sasa, ni Nani hapa anayemjua? Kristo, hiyo ni kweli?

214 Aisee, huyo mtu aliyeketi karibu nawe hapo, ili pia upate kuamini, na kujua ya kwamba mimi ni mtumishi Wake, si mimi, unamwombea mkeo, pia kutoka Georgia. Uwe na ushujaa mwingi, itakuwa sawa.

"Kama unaamini; kama unaweza kuamini." Unaamini? "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

215 Maskini msichana aliyeketi hapa akiomba, mwenye u—ugonjwa wa uti wa mgongo shingoni, papa hapa, unatoka Baton Rouge, Bi. Hantz, simama. Pokea uponyaji wako.

216 Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, hatufahamiani kabisa. Kama hatufahamiani, punga mkono wako, Dada, ili kwamba wajue. Wewe kuwa na imani, na uamini.

217 Huyo hapo yule Malaika amesimama papa hapa nyuma. Mnaiona hiyo Nuru? Hivi hamwezi kuiona Hiyo? Ni mwanamke aliye na tatizo la kiroho. Bibi Haynes, jina lake, Bibi Haynes, amini kwa moyo wako wote. Atakuwa sawa. Unaukubali sasa? Sikujui, sijawahi kukuona.

218 Mama aliyeketi karibu nawe hapo, akiomba pia. Ana shida ya matumbo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani, mama? Bi. Jackson, amini kwa moyo wako wote.

219 Ninaipa changamoto imani yako. Hapa, kama ninyi watu huko kwenye kusanyiko huko nyuma kabisa mnaweza kunisikia, ninyi watu weusi, inueni mikono yenu, juu kabisa.

220 Wa tatu kutoka mwisho hapa nje, huyo mama mweusi anaugua ugonjwa wa figo. Yule aliyeketi karibu naye anaugua ugonjwa wa figo, pia. Unakubali uponyaji wako? Inua mikono yako kama unakubali uponyaji wako. Vema, nenda nyumbani, Kristo anakuponya.

221 Kuwa na imani na uamini, usiwe na shaka. Mungu yupo hapa. Ninyi watu mlio kwenye viti hivyo na kadhalika, siwezi kuwaponya. Mimi . . . Wewe . . . Ninajua ninii . . . Ninaweza kukwambia shida yako ikiwa utaamini, kifafa, polio moja kwa moja mgongoni mwako. Kama unaamini kwa moyo wote, unaweza kusogeza kiti chako, kisha uende nyumbani, uwe mzima, kama unaamini, bali huna budi kuamini kwa moyo wako wote.

222 Ni nani huyu aliyelala hapa kwenye kitanda cha wagonjwa? Mtu huyo? Naam. Hiyo imesababishwa na upasuaji, ulimpofusha. Hiyo ni kweli. Upasuaji wa uvimbe ubongoni, ulimpoozesha, ukamfanya awe katika hali hiyo. Siwezi kuponya, lakini Roho Mtakatifu yupo hapa. Unaamini Malaika wa Bwana yuko katikati ya watu? Je, unamkubali kama Mponyaji wako?

223 Baba yetu wa Mbinguni, ninapowaomba watu hawa wawekeane mikono na kuomba, ninaomba ya kwamba—ya kwamba utathibitisha Neno Lako zaidi kusema jambo hili, ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ninakuomba, Baba, sasa hivi, wakati Uwepo Wako wa Kiungu ukiwa pamoja nasi, jalia kila mtu aliye katika uwepo wa Kiungu, ninavyojisikia mwenyewe kudhoofika, nakuomba Wewe, Baba, mponye kila mmoja wao, jalia wajue ya kwamba ni Wewe. "Msiogope, Ni Mimi," asema Roho Mtakatifu, Chanzo pekee cha msaada wakati wa shida.

224 Njoni, kila mtu, mpokee zeri ya Gileadi, mkachanjwe dhidi ya hofu zote na mashaka, mpokeeni Bwana kama Mponyaji na Mwokozi wenu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

225 Ninamwagiza kila mwanamume hapa ndani, na kila mwanamke, mvulana, na msichana katika Jina la Yesu Kristo, ambaye Uwepo Wake upo hapa, anayejua kwamba hakuna mwanadamu anayeweza kufanya mambo haya duniani, ni kweli, haina budi kuwa ni Roho wa Mungu kabisa, nami ninamwagiza kasisi yeyote kukanusha ya kwamba Biblia haiahidi jambo hili litatukia kabla tu ya wakati wa mwisho. Mnaona?

226 Basi Biblia imetimizwa usiku wa leo. Yesu Kristo, Yule aliyefufuka, Yule mnayemwita Nafsi ya tatu, ni Mtu yule yule, aliye miongoni mwetu sasa akitenda kazi katika mwili wetu, kama Yeye, kama vile Mungu alivyotenda katika mwili wa Mwanawe Mwenyewe, Yesu Kristo, anatenda kazi katika mwili wa watoto waliofanywa wana wenye mamlaka, kupitia Yesu Kristo, kama Yeye alivyoahidi, "Bado kitambo kidogo, na asiyeamini hataniona tena, si mpaka mwisho wa ulimwengu, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari." Huyu hapa usiku wa leo.

227 Nashangaa usiku wa leo, Mbele za huyu Mtakatifu Mkuu, ni wangapi wenu wangetaka maagizo hayo yasemwe juu yenu? Je, ungetaka kuja na kumkubali kama Mwokozi wako? Simama, ushuke chini pamoja nasi, ukabatizwe. Ungefanya hivyo? Tunapoimba wimbo, tafadhalini, *Nampenda.*

228 Sijui kama mtasimama na kuja hapa juu na kusimama, ambapo ninaweza kuomba na kuwawekea mikono, mpate kumpokea Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo unavyompokea Roho Mtakatifu ni kwa kuwekewa mikono, Biblia inasema hivyo. Je, unajua ya kwamba Kristo yupo hapa? Inua mkono wako. "Ni kitu gani kinachotuzuia?" Filipo alimwambia yule towashi, "Nini . . . ?" Ama yule towashi akamwambia Filipo, hasa, "Ni kitu gani kinachotuzuia? Haya hapa maji."

229 Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu," huyo Ndiye mnayemwona akifanya kazi hapa. "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Fuatilia hilo vizuri, uone kitakachotukia; hivyo ndivyo nilivyofanya, na hilo ndilo lililotukia; fanya hivyo, nalo litatukia kwako.

Napenda . . .

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa.

Na . . .

230 Roho Mtakatifu mkuu, Uwepo Wako upo hapa, ukiponya kote jengoni. Sasa jalia wale, Bwana, wasio na Wewe, wasiojua maana ya huyu Roho Mtakatifu mkuu, hawajui hata msamaha wa dhambi zao, jalia waje mbele sasa, Bwana, katika Jina la Yesu, ninaomba.

231 Hivi hutasimama sasa na kuja hapa kwenye Uwepo? Mungu atakuuliza kwenye Siku ya Hukumu, "Nilitokea Shreveport Jumamosi ile usiku, nilihubiri Neno kupitia kwa mtu asiye na elimu, nilihubiri Neno Langu, nilijionyesha Mwenyewe kuwa hai kulithibitisha Neno Langu," nawe utaombwa kutoa sababu, "kwa nini hukuukubali?"

232 Mungu akubariki, ndugu yangu. Njoo papa hapa. Mungu akubariki, dada yangu. Mtu mwingine? Kama mtu hajawahi kubatizwa, bado, katika ubatizo wa Kikristo, hakuna fomula nyingine katika Biblia, hakuna mahali hata kidogo! Kama wewe ni mwenye dhambi, njoo mbele, kama wewe ni mfuasi wa kanisa, njoo mbele.

233 Kama hujawahi kubatizwa kwa maagizo ambayo Petro aliweka katika Matendo 2:38, ninakuagiza mbele za Mungu na Malaika: Mbona mnitilie shaka kama nabii ninaposimama hapa na kuwaambia ukweli, na mnajua ya kwamba nabii ana Neno la Bwana? Hiyo ndiyo ofisi yake ya Kiungu. Nawaambia ukweli. Ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba kila mtu asiye na ubatizo wa maji, umenyunyiziwa, ama njia yoyote, njoo ukapatanishwe na Mungu, uyafuate maagizo. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; milango ya kuzimu haitalishinda kamwe."

> Nampenda . . .

Simama kwa miguu yako sasa uje, sivyo?

> Napenda . . .

Sivyo?

> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua . . .

Njoni sasa! Mbona? Mbona hamji? Kwa nini?

Unasema, "Kanisa langu linaamini katika kunyunyizia. Kanisa langu linaamini jambo lingine."

234 Ninawauliza, "Kwa nini?" kwa maagizo ambayo Mungu alitoa, hakuna agizo lingine katika Biblia kinyume chake. Kama kuna mtu yeyote anayeweza kunionyesha agizo kinyume na hilo kwa ajili ya wokovu, njoo unionyeshe. Halipo. Hayo ni maagizo ya Mungu. Kwa nini hamtanionyesha?

235 Kuna mtu yeyote hapa ambaye amemfuata Mungu katika utaratibu huu? Inueni mikono yenu. Ni wangapi hapa wamemfuata Mungu katika utaratibu huu? Labda ninyi nyote mmemfuata.

236 Kama hujafanya hivyo, basi utaulizwa kwenye Hukumu. Kumbukeni, Mungu yeye yule aliye juu yangu, Roho yeye yule anayeniambia niulize jambo hili, na kutoa changamoto hii, ananiambia sasa Yeye atawauliza kwenye Hukumu, ambayo unaweza kuifikia kabla ya asubuhi: "Kwa nini hukufanya hivyo?" BWANA ASEMA HIVI.

237 Hatuwezi kuigiza kanisa tena. Mungu yuko katikati yetu. Hivi mnahisi kicho hicho cha kutisha? Je, mnajua hiyo ni nini? Ni Roho Mtakatifu akiita, akitenda kazi, akijaribu kuingia ndani. Mara nyingine tena, ili kwamba nitakuwa na hakika kwamba

hakuna damu itakayokuwa mikononi mwangu kwenye Siku ya Hukumu, kumbukeni ninawaagiza mbele za Mungu: Njoni!

Na—nampenda . . .

[Ndugu Branham anawaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . .? . . .

Mungu, katika Jina la Yesu, jalia ajazwe na Roho Mtakatifu.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo jalia yeye . . .? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo jalia ajazwe na Roho Mtakatifu.

Katika Jina la Yesu Kristo jalia ajazwe na Roho Mtakatifu.

Katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . .

Bwana Mungu, uturehemu, uwape ubatizo wa Roho Mtakatifu . . .? . . .

Mwenyezi Mungu, ahadi Yako ya Neno Lako, jalia idhihirishwe katika huyu, ndugu yangu. Jalia ampokee Roho Mtakatifu. Tujalie Bwana.

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . . mjaze dada yangu na Roho Wako.

Vivyo hivyo . . .? . . . mjaze na Roho Mtakatifu . . .? . . . Naweka mikono yangu . . .? . . .

. . . na kumjaza na Roho Mtakatifu, Bwana . . .? . . .

Katika Jina la Yesu Kristo . . .? . . .

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, tafadhali Bwana, sasa, anapokuja apate kubatizwa, jalia awe na maji na Roho pia . . .? . . .

Katika Jina la Yesu . . .? . . .

Vivyo hivyo juu ya ndugu yangu, na apokee . . .? . . . apokee . . .? . . .

Ndugu yangu na ampokee Roho Mtakatifu, imani yake ni Kwako mpaka mauti yatakapomchukua kutoka kaburini, katika Jina la Yesu. Tujalie Bwana.

Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, jalia apokee . . .? . . .

Baba, Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, jalia ampokee Roho Mtakatifu . . .? . . . mambo yote . . .? . . .

Baba wa Mbinguni, Wewe uliyepo sasa, naomba umtume Roho Mtakatifu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo.

Njoo, Dada mpendwa. Njoni—njoni moja kwa moja huku, kila—kila mmoja sasa, papa hapa juu ili . . . Naam, Dada.

238 Baba yetu wa Mbinguni, kwa upako wa Roho Mtakatifu, jalia dada yetu ampokee Roho Mtakatifu. Kama vile Petro

alivyoshuka, na kuwaombea, na kuwawekea mikono, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao, ninaomba ya kwamba wakati anapoupokea ubatizo wake wa maji, Roho Mtakatifu na aje juu yake. Ninaomba, katika Jina la Yesu.

239 Waweza kuja mbele sasa? Simama tu vizuri sana na mtulivu, kwa muda kidogo tu. Vema.

240 Baba wa Mbinguni, wakati huyu kijana anayeonekana mwenye nguvu, anaposimama hapa, naomba, maji yanapomfunika, jalia Roho Mtakatifu amjaze. Jalia atumiwe kwa utukufu Wako, Bwana, ni ahadi Yako. Katika Jina la Yesu. Amina.

241 Nimekosa mmoja, mtu fulani? Nikiwawekea mikono, hiyo ndiyo ahadi:

> *Tubuni* kila mmoja wenu, *mkabatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi* zenu, *nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*
>
> *Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa* watu wote *walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

242 Hayo ndiyo maagizo. Kuna mwingine kabla hatujaomba maombi haya na kwenda kwenye kidimbwi, ambaye hajawahi kubatizwa? Mwingine.

243 Baba mwenye rehema, chini ya upako na sadikisho la Uwepo wa Roho Mtakatifu, mtu huyu anakuja ameinamisha kichwa na moyo wake, anapoupokea ubatizo wa maji, jalia ajazwe na Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

Dada.

244 Ee Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, na Mpaji wa kila karama njema, tuma baraka Zako juu ya dada yangu, jalia ampokee huyu Roho Mtakatifu aliyebarikiwa, anapoenda majini kutii amri Yako. Kupitia Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

245 Loo, ni wakati wenye uchaji jinsi gani! Ho—hofu ya Roho Mtakatifu. Inaonekana tu kama mtu fulani anamhuzunisha. Sijui, labda ni mimi, mnaona, maana, na—natumaini sivyo, kwa sababu nilitoa tamshi baya sana dakika chache tu zilizopita bila kujua, Hata nilijisikia mwenyewe nikilisema, nililiagiza kusanyiko hili mbele za Yesu Kristo kwamba watajibu "Mbona?" kwenye Siku hiyo, mnaona. Hakuna udhuru, mnaona, kwa sababu tayari amejidhihirisha Mwenyewe kwa Neno Lake, kupitia Neno Lake, katika watu Wake, Naye yupo hapa; nionyeshe mahali pengine popote. Unaona? Unaona? Ni hao tu sasa? Mwingine?

246 Loo, njoo, Dada mpendwa, naam, maskini msichana huyu tineja. Dada mwenye imani ya moja kwa moja, nina furaha sana

kujua ya kwamba ulimgeukia Kristo, inanikumbusha juu ya binti yangu mdogo, Rebekah.

247 Ee Bwana Mungu, huwezi kumwacha . . .? . . . jalia ajazwe na Roho Mtakatifu . . .? . . .

248 Baba yetu wa Mbinguni, kungojea huko kulikuwa kunafaa. Ninaomba ya kwamba utambariki dada yangu sasa, mjaze na Roho Mtakatifu anapokutii, akishuka. Anataka kuchanjwa aondokane na hofu na mahangaiko ya maisha. Jalia Roho Mtakatifu, ile Chanjo kuu ya Mungu, iondoayo dhambi, jalia iingie maishani mwake na kumwongoza kote katika safari yake. Kupitia Jina la Yesu.

Baki tu papo hapo kwa muda kidogo tu, Dada.

249 Hilo limekwisha? Kila mtu sasa? Kumbuka kila mtu anahisi sasa kwamba . . . Liwazie tu, rafiki. Nina hakika kama kweli tungeweza, tungekuwa na namna fulani tu ya kitu fulani tungeweza kukibana kwa mikono yetu, na kutambua yale yanayotendeka hapa sasa! Ha—hatujui jambo hilo. Ni—ninasema mambo haya labda kwa mafumbo kwenu, labda hu—hulielewi, lakini kama ninyi, ningeweza tu kuwaruhusu mpate kile ni—ni—nijuacho sasa, kile ninachohisi sasa, na kujua kilichopo! Saa kuu ya uamuzi, kanisa hili limefikia saa yake, limefika kwenye Mlima wake wa Kugeuka Sura katika ushirika huu.

250 Mambo yametukia ambayo hata hayajawahi kuwaziwa, bali ilitabiriwa muda mrefu uliopita yangetukia. Hii ndiyo saa ya uamuzi kwa wengi; nina furaha sana kwamba hawa wamekuja. Wazia jambo hilo, Roho Mtakatifu mkuu wa Mungu, aliyekutana na baba Ibrahimu huko nje, ameshuka akaja miongoni mwetu, akifanya kazi katika maisha ya wanadamu, kila mmoja wetu akitembea kwenye jengo hili, yale hasa aliyosema angefanya.

251 Tunaona ile mikutano mikuu na makongamano yaliyonenwa miaka elfu mbili mia tano iliyopita yakitukia tu juma moja ama mawili yaliyopita, tunaona wakati wa atomiki. Nilikuwa nikinukuu jana usiku unabii niliopewa huko nyuma mwaka wa 1933 wa mambo saba ambayo yangetukia: Ujerumani, Ngome ya Siegfried, na uchaguzi wa Rais, na mambo haya mengine yote. Matano ya hayo tayari yametukia, mawili yamesalia, kule kuja kwa utawala wa mwanamke mmoja Marekani kuchukua mamlaka, labda kanisa kuchukua mamlaka litawale. Angalieni, ni BWANA ASEMA HIVI.

252 Ndipo nikawaona wakiunda motokaa ambayo haikuhitaji usukani ndani yake. Niliona ile Ngome ya Maginot ilikuwa, badala ya ile Siegfried, ile Ngome ya Maginot miaka kumi na mmoja, na kuwaambia watu, imeandikwa kwenye karatasi. Yeye hajawahi hata wakati mmoja, ninamwagiza mtu yeyote katika uwepo wa Kiungu, ama ulimwenguni, kuniambia wakati mmoja ambapo Roho Mtakatifu aliwahi kunena na kusema mambo haya

ambapo hayakutimia. Mnaona? Hiyo ni kweli. Loo, ni saa ya jinsi gani tunayoishi! Ni wakati wa jinsi gani sasa hivi, utulivu kama wa mauti mahali fulani. Mnaona?

253 Sasa, mimi . . . Kuna mwingine? Kuna mtu mwingine ambaye angetaka kuja wakati huu, angetaka kuja hapa, na kusema, "Sijawahi kumpokea Roho Mtakatifu, Ndugu Branham. Mimi—mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa, sijawahi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, nimenyunyiziwa," ama kumwagiliwa, ama chochote zaidi, "lakini na—nataka kuja kulingana na vile Biblia inavyoniambia. Sioni haya, na—na—namtaka Kristo, naja sasa hivi"?

254 Nitasema tu, mara nyingine tena tutaimba, na tukumbuke basi mpaka kesho asubuhi basi. Kisha tutawapeleka wasikilizaji hawa hapa moja kwa moja kwenye orofa ya chini. Nafikiri kila kitu kiko tayari, na mahali pa kubatizia pamejazwa, nasi tuko tayari kuingia katika ubatizo tu . . .

Huyu hapa mtu mmoja zaidi. Mungu akubariki, Dada, njoo hapa. Ninapenda kuwawekea watu mikono kwa sababu Biblia inatuagiza kufanya hivyo. Angalieni.

255 Baba wa Mbinguni, jalia apokee baraka za Mungu. Anashuka, sasa, kwenye kitu ambacho ni BWANA ASEMA HIVI. Mpe, Bwana, utoshelevu, chanjo hii tuliyonena habari zake kwa njia hiyo, Baba. Ninaomba, katika Jina la Yesu.

. . . Yesu kwa huruma . . .

Mungu awabariki.

256 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba pia utampa ndugu yetu chanjo hii tunayozungumzia. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aipokee. Amina.

Mungu akubariki sasa, Ndugu.

257 Baba wa Mbinguni juu ya msichana huyu mdogo, nakuomba Wewe . . .? . . . katika Jina . . .? . . .

60-1126 Kwa Nini?
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.



Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org